# Nipashe
MWANGA WA JAMII

Alhamisi Desemba 3, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580418

www.ippmedia.com



www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


**Familia** yafunguka Hoteli Ngurdoto kugeuzwa hosteli



UKURASA 3

**Wenye** VVU watakiwa kuwaonyesha wapenzi wao ili wapewe dawa

UKURASA 16



ama

ALHAMISI DESEMBA 3, 2020

AFYA NA MAZINGIRA

Shinyanga inavyochechemea ndani ya tope zito la utapiamlo sugu kwenye mkoa

Ukurasa 13

Pwani katika vikumbo kujichomoa utapiamlo

Ukurasa 14

AFYA

## Kangaroo; mbinu inayofuta robo vifo vya njiti walioko hospitalini

• Mzaliwa hali hiyo ajitosa kuwapigania

Na Christina Mwakangale

KUZALIWA njiti, haijegemei historia ya mama kutoka familia duni au la. Inatokea pale kunapokuwapo hitilafu yeyote wakati wa ujauzito.

Kimataifa, Tanzania inashika nafasi ya 20 kwa kuwa na watoto wengi wanaozaliwa njiti, jumla yao wako 213,000 kila mwaka na kati yao njiti 40,000 wanafariki ndani ya kipindi hicho kutokana na matatizo mbalimbali, ikiwamo upumuaji duni.

Pia, ni kati ya nchi 10 duniani zinazochangia asilimia 66 ya vifo vya watoto wachanga, kutokana na matatizo mbalimbali ikiwamo uzito mdogo. Kwa mujibu wa wataalamu wa afya mimba huchukua wiki 38 hadi 42 mtoto kuzaliwa.

Kangaroo ni mtindo unaotumiwa na kitengo cha kulea watoto njiti kilichopo Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kwa kuiga namna ya malezi ya mnyama aitwaye Kangaroo, anayemhifadhi mtoto wake katika mfuko wa asili uliopo nje ya tumbo na kumfanya mtoto kupata joto muda wote.

Mtoto anayezaliwa chini ya miezi tisa na uzito mdogo, kiafya anapaswa kutumia kangaroo nyumbani au akiwa hospitalini na kuwekewa vifaa vya upumuaji.

Mganga Bingwa wa Watoto na Watoto Wachanga hadi vijana umri miaka 28, kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Augustine Massawe, ameiambia Nipashe kwamba utafiti uliofanywa mapema mwaka huu na hospitali hiyo, umeonyesha kangaroo imepunguza vifo vya watoto njiti kwa asilimia 25.

Dk. Deborah Maufi, mdau katika vita vya kuokoa watoto njiti.

Doris Mollel; alizaliwa mapacha njiti, leo yuko mstari wa mbele vitani kuwaokoa. **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE**

**MBINU ZA KUWAOKOA**

Anasema utafiti huo, MNH kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) kwenye nchi tano ikiwamo Tanzania, Ghana, Malawi, Nigeria na India, umebaini mtindo huo utaokoa vifo vya watoto hao kwa nchi zinazoendelea, ambazo kwa kiasi kikubwa hushindwa kumudu gharama za matibabu, vifaa vya kuhudumia kabla ya uzazi, ikiwamo anachokiita 'incubators' katika kila hospitali nchini.

Dk. Massawe anataja vifaa vingine, ni mipira ya kupumua, hewa ya oksijeni, dawa za kukomaza mapafu na kwamba njia ya kangaroo haina gharama.

Kwa sababu mama mwenye mtoto njiti, anatajwa kuwa na uwezo wa kutumia nguo za asili, kikiwamo kitenge kwa kumbeba mtoto wake na kumpa joto.

"Niliandika 'proposal' (hoja) hapa MNH na kusimamia hii study (mapitio kitaalamu) iliyomalizika Februari mwaka huu, katika nchi hizo tano pamoja na WHO.

"Tunafuatilia watoto walioingia katika utafiti huu, kwamba Kangaroo inasaidiaje. Zamani ilikuwa unangoja mtoto awe 'stable' (amekoma) ndio umpeleke kwa mama yake.

"Hivi sasa hata kama anahema kwa shida, anakaa na mama yake akimbeba kwa mtindo wa kangaroo, tunataka hadithi ya theluthi moja ya watoto wanazaliwa njiti. Tunahitaji sehemu ya kutunza watoto iwe kila hospitali. Mkoa wa Dar es Salaam wanazaliwa watoto njiti 2,000," anasema.

Massawe, anasema kwa miaka miwili iliyopita, MNH ilifanya utafiti na ilionekana njia hii ni nzuri na njia hiyo ya mama kubeba mtoto 'ngozi kwa ngozi' hata kama mtoto atahitaji oksijeni, imetafitiwa ikaonekana asilimia 25 ya watoto hawa 'wamesurvive' (wamesalimika) kutokana na nyenzo kangaroo.

**SABABU NJITI**

Dk. Massawe anataja kuwapo mengi yanayosababisha mtoto kuzaliwa kabla ya muda, ikiwamo mjamzito kuugua maradhi kama malaria, presha, kifua kikuu na mkojo mchafu 'UTI', kisukari, upun-

INAENDELEA UK.12

UKURASA 11

# Padri kortini tuhuma kumbaka mwanafunzi

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**KIKWETE AWATAKA WAHITIMU KUWA WAZALENDO WA TAIFA**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete, amewataka...

UKURASA WA 4

**RC ASITISHA LIKIZO ZA MA-DC NA MA-DED**

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amesitisha likizo za...

UKURASA WA 5

**MWALIMU MBARONI MADAI KUKUTWA NA MWANAFUNZI**

JESHI la Polisi mkoani Songwe, linamshikilia mwalimu wa Shule ya...




Mkuu wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE), Rais mstaafu, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete (kushoto), akifurahia jambo na Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, wakati wa maandamano ya mahafali ya 12 ya chuo hicho, mjini Iringa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

## TAKUKURU yaokoa fedha mikopo umiza asilimia 300

UKURASA 3

## Mratibu BAVICHA asimulia walivyotolewa usiku gerezani

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play
Download on the App Store



**MICHEZO** **SIMBA YAJA NA TIKI-TAKA KWA MKAPA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA



Mratibu wa Uhamasishaji wa Baraza la Vijana Taifa la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAVICHA), Twaha Mwaipaya, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mwenendo wa kesi iliyokuwa ikiwakabili mpaka kufutiwa mashtaka. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Padri kortini tuhuma kumbaka mwanafunzi

**Na Daniel Sabuni,** HAI

PADRE wa Kanisa Katoliki, Paroki ya Manushi, Jimbo la Moshi mkoani Kilimanjaro, Erasmus Swai (44), amefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Hai akituhumiwa kumbaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wa miaka 17 wa kidato cha nne Shule ya Sekondari Kimaseki Arusha (jina linahifadhiwa).

Hata hivyo, kiongozi huyo wa kiroho kwa sasa amesimamishwa majukumu ya utumishi wa kanisa, hivyo kurudi kijijini kwake Msufini Uru, wilayani Moshi Vijijini.

Padri Swai anayekabiliwa na kesi namba 159 ya Mwaka 2020 na alifikishwa mbele ya Hakimu wa Mahakama hiyo, Thurston Kombe na kusomewa mashtaka mawili.

Mashtaka hayo ni kubaka chini ya kifungu 130 cha Sheria ya 2002 na kumpa mwanafunzi ujauzito chini ya kifungu no. 60A cha sheria ya elimu.

Awali, ilidaiwa na Mwendesha Mashtaka wa Polisi, Lobulu Mbise, kuwa Machi, mwaka huu katika Hoteli ya Snow view katika Mji wa Boman'gombe wilayani Hai kwa nyakati tofauti, Padre Swai alimbaka mwanafunzi huyo.

Alidai kuwa mshtakiwa alimpeleka katika Hoteli moja na kukodisha chumba na kumrubuni mwanafunzi huyo na kwamba na baada ya miezi mitatu aligundulika kuwa na ujauzito.

Hata hivyo, baada ya kusomwa kwa mashtaka hayo, Padri Swai alikana na ndipo hakimu alieleza kuwa dhamana iko wazi.

Mtuhumiwa alitimiza masharti ya dhamana kwa kuwa na wadhamini wawili wanaofahamika na kumdhamini kwa Sh. 2,000,000. Kesi hiyo imepangwa kutajwa tena Desemba 17, mwaka huu.


**bgtl BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **NMB BANK** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa wadaiwa wanaotajwa hapo chini, walipe madeni wanayodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) zilizodhamini mikopo yao kwa **MNADA WA HADHARA.** Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE | TAWI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | IRENE GRIMBE RUHIKURA | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye Kiwanja chenye **Hati ya** mauziano maeneo ya Dovya Manispaa ya **Temeke** kwa jina la **Salma J hamis** | 19/12/2020 | CONGO |
| 2. | GERALD SADOCK SICHALWE | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye Kiwanja chenye **Hati** ya mauziano maeneo ya yange yange Manispaa ya Ilala iliyopo kwa jina la Charles Donald Fumbo | 16/12/2020 | CONGO |
| 3. | HAJI RASHID ISMAIL | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye **Kiwanja** chenye **Hati** ya mauziano maeneo ya Ponde Twangoma Manispaa ya Temeke. | 19/12/2020 | ILALA |
| 4. | PETER WAMBURA KIMORI | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye **Kiwanja** chenye **Hati** ya Mauziano maeneo ya Zogo Ali Manispaa ya ilala | 16/12/2020 | AIRPORT |
| 5. | JUMANNE DANIEL NDENZAKO. | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye **Kiwanja** chenye **Hati** ya Mauziano maeneo ya **Malamba Mawili** Manispaa ya **Ubungo** kwa jina la **Jumanne Daniel Ndezako** | 23/12/2020 | AIRPORT |
| 6. | ELIASA HAJI TENGENEZA | Nyumba ya Makazi iliyopo mtaa wa kibonde maji B kwenye **Kiwanja** chenye **Hati** ya Mauziano Wilaya ya **Temeke** kwa Jina la **Eliasa Haji Tengeneza** | 19/12/2020 | MBAGALA |
| 7 | IZACK ERNEST | Nyumba ambayo haijakamilika iliopo kwenye kiwanja chenye Hati ya mauziano maeneo ya Kimara Temboni inayosomeka kwa jina la **Genoveva Ndenumbi** Manispaa ya **Ubungo**. | 23/12/2020 | AIRPORT |
| 8 | SALUM SHADHIRI SALUM | Nyumba ya Makazi iliyopo kwenye **Kiwanja** chenye **Hati** ya Mauziano maeneo ya **Malamba Mawili** Manispaa ya **Ubungo** kwa jina la **Salum Shadhiri Salum** | 23/12/2020 | AIRPORT |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na: AU**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**NMB Bank PLC,**
**Ohio Street / Ali Hassan Mwinyi Road,**
**P.O. BOX 9213,**
**DAR ES SALAAM**
**Telephone: +255 22 2322550**
**email: Benedicto.Baragomwa@nmbbank.co.tz**

216025501


## Mratibu BAVICHA asimulia walivyotolewa usiku gerezani

**Na Elizabeth Zaya**

MRATIBU Mwenezi wa Baraza la Vijana la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (BAVICHA) Taifa, Twaha Mwaipaya, ameeleza jinsi yeye na aliyekuwa Katibu Mkuu wa Baraza hilo, Nusrat Hanje, walivyoachiwa kutoka gerezani usiku.

Kadhalika, ameeleza mahabusu mwenzake alivyowatoroka siku moja baada ya kutolewa na kwenda kuapa bungeni na wao kushuhudia kupitia runinga.

Nusrat ni miongoni mwa wabunge 19 wa CHADEMA waliovuliwa uanachama na chama hicho kwa sababu ya kwenda kuapa ubunge wa viti maalum, kinyume na makubaliano ya chama chao.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mwaipaya alisema baada ya kutolewa mahabusu Novemba 23, walikokaa kwa zaidi ya siku 100, Nusrat hakupenda kujumuika na wenzake licha ya kuchukuliwa na Mwenyekiti wa Baraza hilo Mkoa wa Dodoma, kumwomba akapumzike nyumbani kwake.

"Baada ya kutolewa mahabusu, tuliwapigia simu viongozi mbalimbali wa Baraza akiwamo Mwenyekiti wetu Mkoa wa Dodoma, Aisha Madoga, ambaye baada ya kuja aliondoka na Nusrat kwenda kupumzika nyumbani kwake," anasimulia Mwaipaya. "Lakini baada ya kufika nyumbani kwa mwenyekiti wetu, alikataa kulala tena pale kwake, akasema ataenda hotelini kwa sababu anahofia kwamba anaweza kukamatwa tena, na hivyo akaruhusiwa kwenda."

Mwaipaya alisema Novemba 26, saa tatu asubuhi, alipiga simu kwa Mwenyekiti wa Baraza hilo Mkoa wa Dodoma ambaye aliondoka na Nusrat kwenda kupumzika ambaye alimwambia hakuwa nyumbani kwake, alilala hotelini ambako na amepata taarifa kwamba alishatoka na hajulikani alikokwenda.

"Kwa kweli taarifa zile zilinishtua kwa sababu tulikuwa tumekubaliana kwamba asubuhi kabla ya kurejea Dar es Salaam tungekuwa na kikao cha kuzungumza kidogo na kuagana na wenzetu wengine tuliokuwa nao."

"Lakini baadaye tulipata taarifa kwa walinzi kwamba alifuatwa pale hotelini na viongozi wawili wa CHADEMA wanawake japokuwa nao tulipowapigia walikana kuondoka naye. Taarifa zile kwa kweli zilileta taharuki, tukawa tunawaza sijui ametekwa au kakumbwa na jambo gani baya. Tulianza kumtafuta bila mafanikio."

"Lakini baadaye kidogo tulianza kusikia tetesi kwamba, kuna wabunge wa CHADEMA ambao wanatarajiwa kuapishwa na Nusrat naye akitajwa kuwa ni miongoni mwao. Tulishtuka sana na hapo nilikumbuka kwa sababu kuna siku tukiwa mahabusu aliwahi kuniambia kwamba amepelekewa fomu mahabusu ili ajaze kwa ajili ya viti maalum, na ndio nikaamini kumbe ilikuwa kweli."

Mwaipaya, Nusrati na wenzao sita, waliachiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Novemba 23.

**DPP AJIBU**

MKURUGENZI wa Mastaka Nchini (DPP), Biswalo Mganga, amejitokeza hadharani na kujibu malalamiko yanayoikabili ofisi yake kumfutia mashtaka kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Nusrat Hanje, aliyekaa mahabusu siku 163.

Katika majibu yake, alisema hakuna muda maalumu kisheria unaomtaka kumtoa mahabusu kutoka gerezani.

Aliyasema hayo jana wakati akiwaachia mahabusu 72 wakiwamo wanawake 10 na wanaume 62 katika Gereza Kuu la Karanga mjini hapa, baada ya kufanya ukaguzi kwa siku mbili na kusikiliza kero za wafungwa na mahabusu.

"Yako malalamiko kuwa mwanachama wa CHADEMA kaachiwa bila utaratibu. Kesi nimeifuta mimi DPP kwa mamlaka niliyo nayo kisheria kwa kifungu 91 cha CPA cha 2002 kwa mujibu wa makosa ya jinai," alisema Mganga.

**HABARI KITAIFA**

# TAKUKURU yaokoa, kurejesha mamilioni ya walimu wastaafu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilayani Kahama, Mkoa wa Shinyanga, imeokoa na kurejesha Sh.milioni 23.6 za walimu wastaafu 19 walikopo kutoka kwa wakopeshaji wa mikopo yenye riba kubwa.

Walimu hao pia walikuwa wadaiwa sugu Chama cha Akiba na Mikopo cha Walimu (SACCOS).

Akikabidhi fedha hizo jana kwa walimu wastaafu 19 kutoka Halmashauri ya Kahama Mjini na Msalala, Kamanda wa TAKUKURU wilayani Kahama, Cosmas Shauri, alisema fedha hizo zilikopeshwa kwa wakopeshaji wawili wa mikopo, Cleophance Credit and Investment na Super Salo Investment L.T.D.

Alisema Sh. 15,410,000 zimeokolewa toka kwa wakopeshaji wa mikopo yenye riba kubwa ya asilimia 300 kwa kumkopesha Mwalimu Paulina Malecha huku Sh. 8,200,000 zikiokolewa toka kwa wadaiwa sugu wa Chama cha Akiba na Mikopo cha Walimu Kahama SACCOS Ltd.

Aidha, Shauri alisema kampuni ya ukopeshaji ya Super Salo Investment Ltd, ilikopesha Sh. 9,760,000 na sh. 5,650,000 fedha ambazo ni za mwalimu mstafu Paulina Malecha aliyekuwa mwalimu katika Shule ya Msingi Nyahanga.

"Julai mwaka huu tulikabidhi fedha kwa walimu wastaafu toka kwa Walimu Saccos na leo (jana) tunakabidhi Sh. milioni 23.6 kwa walimu wastaafu 19, mmoja kutoka Halmashauri ya Msalala na 18 Kahama Mjini,"alisema Shauri.

Nae Paulina Malecha, Mwalimu mstafu shule ya msingi Nyahanaga alisema aliiingia kwenye mikopo yenye riba kubwa ya asilimia 300 baada ya mumewe kupooza na kutafuta fedha za matibabu, na kwamba bila kuwapo kwa maradhi ndani ya familia yake, asingejiingiza kwenye mikopo hiyo.

Mwenyekiti wa Walimu Kahama SACCOS Ltd, Buya Mipawa, aliishukuru TAKUKURU kwa kuokoa kiasi hicho cha fedha, akuahidi kuendelea kushirikiana nayo katika mapambano ya kuokoa fedha za walimu wastaafu, ambao wamekuwa wakidhulumiwa.

# Familia yafunguka Ngurdoto kugeuzwa hosteli

**Na Allan Isack,** ARUMERU

FAMILIA ya aliyekuwa mfanyabiashara maarufu mkoani Arusha, na mmiliki wa hoteli ya kitalii ya Ngurdoto Mountain Lodge, Melau Mrema, imetoa ufafanuzi kuhusu hoteli hiyo kugeuzwa kuwa hosteli ya wanafunzi.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, mtoto wa Mrema, Michelle, alisema hoteli hiyo haijapangishwa bali kuna wanafunzi na wageni wengine wanasubiria mahafali yafanyike na baada ya hapo wataondoka.

"Wageni ni wanafunzi kuna video walipiga huku wakidai kuwa hoteli imegeuzwa kuwa hosteli wakati si kweli. Hapo wapo kwa muda na wataondoka," alisema Michelle.

"Pia leo (jana) hotelini tumewapokea wageni wa masuala ya engineering (uhandisi), kwa hiyo kile kinachozungumzwa kwenye mitandao ya kijamii na baadhi ya watu kuwa hoteli imekuwa hosteli siyo kweli," aliongeza.

Pia alisema kutokana na taarifa hizo kuwa si za kweli, hivi karibuni wataitisha mkutano na waandishi wa habari kueleza ukweli juu ya suala hilo.

Ngurdoto ni hoteli yenye hadhi ya nyota tano, iliyoko wilayani Arumeru, mkoani Arusha na ilikuwa ikimilikiwa na mfanyabiashara Mrema, aliyefariki mwaka 2017. Hoteli hiyo ilifunguliwa rasmi mwaka 2003 ikiwa na vyumba 300 vya kulaza wageni wenye hadhi ya wakuu wa nchi saba na wasaidizi wao.

Wakati wa uhai wake, Mrema alikuwa anamiliki mali nyingine kama hoteli za Naura Spring, Impala na kampuni ya utalii ya Classic Tours Safaris zilizoko mkoani Arusha na Moshi mkoani Kilimanjaro.

Hoteli ya Ngurdoto itaendelea kukumbukwa kutokana na kupokea wageni kutoka maeneo mbalimbali duniani katika mkutano wa Sullivan mwaka 2008.

Katika kipindi cha awamu ya nne, hoteli hiyo ilitumiwa na serikali kwa kufanyika semina elekezi kwa viongozi wote walioteuliwa wakiwamo mawaziri, makatibu wakuu na watendaji wengine.

Ngurdoto pia itakumbukwa kama hoteli pekee iliyokuwa ikifanyika mikutano ya wakuu wa nchi za Afrika ya Mashariki, hasa kutokana na kuwa na vyumba maalumu ambavyo vilikuwa na uwezo wa kulaza marais na kuwa na kumbi kubwa zenye uwezo wa kuchukua zaidi ya wajumbe 2,000 wakati mmoja.

Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), Prof. Eliaman Sedoyeka, juzi alinukuliwa na chombo kimoja cha habari akisema chuo hicho kimekodi hoteli hiyo na zaidi ya wanafunzi 1,000 wamepata sehemu za kulala.

Prof. Sedoyeka alisema chuo hicho kililazimika kutafuta eneo la hosteli baada ya mwaka huu wa masomo kupokea idadi kubwa ya wanafunzi.

"Chuo baada ya kuona ongezeko la wanafunzi, tulianza mkakati kutafuta eneo la kulala wanachuo, tulizungumza na kampuni Landmark ambayo inasimamia hoteli ya Ngurdoto na mazungumzo yaliyokwenda vizuri," alisema.

Aidha alisema kuna mabadiliko yameanza kufanyika ili kupokea wanafunzi wengi ikiwepo kutengenezwa kwa vitanda vya kulala watu wawili wawili (double deka).

"Baada ya mabadiliko tumewapatia vyumba vya kulala wanachuo 1,000 lakini uongozi wa hoteli unaeleza kuna uwezekano wa wanafunzi 2,000 kupata nafasi hivyo tunaendelea na maboresho," alisema.

Alisema makubaliano waliyofikia ni kuwa kwa mwaka mmoja wanafunzi hao, watalazimika kulipia fedha kiasi cha sh.400,000 kwa mwaka.

Vile vile alisema wanachuo watapata sehemu ya kula hapo hapo na mazungumzo yameanza kupata madarasa kutokana na hoteli kuwa na kumbi nyingi zinazofaa kutumika kama madarasa.

Pia alisema hadi juzi chumba cha kompyuta kimefungwa katika hoteli hiyo, wanafunzi wanaweza kuendelea na masomo.


**MUCOBA BANK PLC**
P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.
E-Mail: mucoba@mucobatz.com

## TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MOJA (21) WA WANAHISA WA BENKI YA MUCOBA

Taarifa inatolewa kwa wanahisa kwamba, Mkutano Mkuu wa ishirini na moja wa Wanahisa utafanyika siku ya Jumatano tarehe 23 mwezi wa Disemba 2020 katika ukumbi wa MAM –uliopo Mafinga Mjini kuanzia saa tatu kamili asubuhi.

Ajenda ya Mkutano itakua kama ifuatavyo:

1. Kufungua Mkutano
2. Kuthibitisha Akidi ya Wajumbe
3. Kuchagua Mwenyekiti wa Mkutano
4. Kuridhia ajenda za Mkutano
5. Kuthibitisha Muhtasari wa kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 20 wa Wanahisa uliofanyika tarehe 30.11.2019 na mkutano wa dharura uliofanyika tarehe 11.4.2020
6. Kupokea,kujadili na kuridhia utekelezaji wa yatokanayo na Mkutano Mkuu wa 20 wa Wanahisa uliofanyika tarehe 30.11.2020
7. Kupokea na kujadili taarifa ya Mwenyekiti wa bodi ya Wakurugenxi ya Mwaka 2019.
8. Kupokea na kujadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Mwaka ulioshia tarehe 31.12.2019
9. Kupokea na kujadili mapendekezo ya Mkaguzi huru wa hesabu za benki kwa mwaka 2019
10. Kupokea na kujadili gawio kwa mwaka ulioishia tarehe 31.12.2019
11. Kupokea na kuidhinisha pendekezo la Malipo ya wajumbe wa Bodi
12. Kuwasilisha taarifa kuhusu mashauri yahusuyo Benki
13. Kupokea na kuidhinisha uteuzi wa wakaguzi wa nje wa hesabu kwa mwaka 2019
14. Kufunga Mkutano.

**Notisi hii imetolewa leo tarehe 02/12/ 2020**

**Mambo ya kuzingatia**

1. Mwanahisa anayetarajia kuhudhuria Mkutano huu atatakiwa kufanya hivyo kwa gharama zake mwenyewe; na atatakiwa
2. Iwapo Mwanahisa anayeruhusiwa kuhudhuria Mkutano na kupiga kura, atashindwa kwa sababu zozote zile kuhudhuria Mkutano, ataruhusiwa kuchagua Mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata na kuzingatia taratibu na sheria za Kampuni.

3. Nakala za Makabrasha ya Mkutano zitapatikana pia kwenye ofisi yetu kuu iliyopo Mafinga- Iringa.

**KWA AGIZO LA BODI YA WAKURUGENZI**
**PHILIP RAYMOND PHANUEL**
**KATIBU - BODI YA WAKURUGENZI**



Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga, Cosmas Shauri (kushoto), akikabidhi Sh. milioni 15.4 kwa Mwalimu mstaafu Paulina Malecha, wilayani humo jana, zilizookolewa na taasisi hiyo, baada ya kuchukua mkopo kwa wakopeshaji wa mikopo yenye riba kubwa 'umiza'. **PICHA: SHABAN NJIA**

# JK awataka wahitimu kuwa wazalendo wa taifa

**Na Francis Godwin**, IRINGA

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete, amewataka wahitimu wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa (MUCE) kufanya kazi kwa bidii na kuwa wazalendo kwa taifa.

Kikwete ambaye ni Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alitoa wito huo jana wakati akiahirisha mahafali ya 12 ya chuo hicho ambacho ni Chuo Kikuu Kishiriki cha UDSM.

Alisema wahitimu hao wanao wajibu wa kwenda kuitumia elimu waliyoipata chuoni hapo kwa maendeleo na kuwa wazalendo kwa taifa . "Naomba niwatakie kila la heri wahitimu wote ambao mmehitimu leo (jana) na mkawe na maisha mema zaidi huko mwendako," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Usimamizi ya Chuo hicho na Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. Wiliam Anangisye, aliwataka wahitimu hao kwenda kutanguliza dhamira ya kujiendeleza zaidi kielimu. "Tuko katika dunia yenye ushindani mkubwa wa maarifa hasa pale tunapotaka kufanikiwa zaidi. Ninaamini mkiwa na shauku ya kupenda kujisomea na kujiendeleza kielimu, mtahimili ushindani uliopo katika soko la ajira kitaifa, kikanda na kimataifa," alisema.

Pia aliwataka kutumia elimu waliyoipata kutatua changamoto mbalimbali ili kuboresha hali ya maisha na kujenga jamii badala ya kuibomoa na kuwa pale inapobidi wakajitolee kufungua milango ya fursa zingine.

Alisema kwa kufanya hivyo, watakuwa wameipenda nchi na kuonyesha uzalendo wa kweli kwa kutimiza ndoto za mwasisi wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, aliyewahi kusema kila aliyepata elimu, ana wajibu wa kuwasaidia Watanzania wengine ambao hawakupata bahati ya elimu, lakini walijinyima ili wachache wasome.

Prof. Anangisye alimpongeza Dk. Kikwete kwa usimamizi mahiri wa chuo hicho uliofanya kuwa na mafanikio makubwa zaidi. Pamoja na kumpongeza Dk. Kikwete, alisema serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri ya miundombinu ya elimu nchini, hivyo wanaendelea kumshukuru zaidi na kupongeza ufuatiliaji wake katika sekta ya elimu.

# RC asitisha likizo za ma-DC na ma-DED

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, amesitisha likizo za wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri za mkoa huo, hadi watoto waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza watakapokuwa wameanza masomo Januari 11, mwakani.

Ndikilo alitoa agizo hilo jana wakati akiweka jiwe la msingi katika Shule ya Msingi Chatembo, Kata ya Mwandege wilayani Mkuranga.

Alisema viongozi hao wanatakiwa kuhakikisha vyumba vya madarasa na madawati vinakamilika na kuwawezesha wanafunzi waliofaulu kujiunga na kidato cha kwanza wote wanapata nafasi.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Mkoa wanafunzi waliofaulu katika mkoa ni 30,197 na wanaotakiwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa Wilaya ya Mkuranga ni 7,360.

"Maelekezo yangu haya yatawahusu pia walezi wa wilaya nao hawatakuwa na likizo. Tujitahidi watoto waliofaulu wote wapate nafasi ili waliofaulu waone ni neema si adhabu," alisema.

Katika hatua nyingine, Ndikilo amemwagiza Meneja wa Tanesco Mkuranga kuhakikisha shule ya Chatembo, inaunganishiwa umeme mapema na kwamba itakapofunguliwa Januari, umeme uwe unawake.

Pia alimtaka Meneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) kusimamia ukarabati wa barabara inayofika katika shule hiyo ili kuondoa kero ya madimbwi yanayohifadhi maji katikati ya barabara.

"Ikifika Januari nipate taarifa ya ukarabati wa barabara hii. Nimeishuhudia ubovu uliopo na nitakapoitisha kikao cha bodi ya barabara nipate majibu. Kama utakuwa bado hujatekeleza usifike kwenye hicho kikao," alisisitiza.

Awali, Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Jesi Mpangala, alisema ujenzi wa shule hiyo ulianza Septemba, mwaka huu, na kwa sasa umefikia hatua za umaliziaji.

Alisema Sh. milioni 400 kutoka serikali kuu zilitolewa kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo yenye vyumba 14 vya madarasa, jengo la utawala, matundu ya vyoo vya wanafunzi na walimu, na nyumba za walimu.

Mpangala alisema ifikapo Januari, zaidi ya wanafunzi 2,000 watahamia katika shule hiyo kutoka Shule ya Msingi Mwandege na kipaumbele kitakuwa kwa wale wanaoishi maeneo ya karibu na shule.

# Maonyesho ya bidhaa za viwanda kuanza leo

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Viwanda na Biashara kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tan-Trade) imeandaa Maonyesho ya Tano ya Bidhaa za Viwanda vya Tanzania yatakayoanza leo hadi Desemba 9, mwaka huu. Taarifa iliyotolewa jana na TanTrade ilisema uanzishwaji wa maonyesho hayo, ulilenga ujenzi wa uchumi wa viwanda unakuwa na matokeo chanya katika uchumi na yanayoonekana. Aidha, taarifa ilisema maonyesho haya yanalenga kujenga jukwaa kwa wadau wa sekta ya viwanda kupata fursa ya kujadiliana, kubadilishana uzoefu na kutangaza fursa zilizopo katika sekta hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo iliyotolewa na Mkuu wa Kitendo cha Mawasiliano wa TanTrade, maonyesho hayo pia yanalenga kuvitambua viwanda vya Tanzania na bidhaa zinazozalishwa nchini ili Watanzania wazitambue na kupenda kuzitumia.

"Pia yanalenga kuhamasisha Watanzania kutumia bidhaa na huduma zinazozalishwa hapa nchini na kuwaunganisha wenye viwanda na wazalishaji mbalimbali wa malighafi na huduma zingine zinazotumika viwandani. Kadhalika kuwaunganisha wenye viwanda na wasambazaji wa teknolojia za viwanda," alisema.

Kaulimbiu ya maonyesho hayo, kwa mujibu wa taarifa hiyo ni "Tumia Bidhaa za Tanzania, Jenga Tanzania" ikiwa ni kuhamasisha Watanzania waendelee kupenda, kununua na kutumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya Tanzania. Alisema kwa kufanya hivyo, kutachochea uzalishaji katika sekta mbalimbali za kiuchumi ili kukuza soko la ndani na hatimaye kuiwezesha Tanzania ambayo imeingia katika uchumi wa kati.

Pia maonyesho hayo yatakwenda sambamba na matukio mbalimbali ikiwamo kati ya Wizara ya Viwanda na Biashara, wamiliki wa viwanda nchini na taasisi za uthibiti utakaofanyika Desemba 5, mwaka huu.

Desemba 7, kutakuwa na kongamano la biashara litakaloeleza fursa za biashara katika nchi za Dubai, Falme za Kiarabu na Kuwait litakalokwenda sambamba na mikutano ya biashara ya ana kwa ana (B2B Meeting).

Taarifa hiyo iliotanabaisha kwamba mabanda yatafunguliwa saa 4:00 asubuhi hadi saa 12 jioni na hakutakuwa na kiingilio.

HABARI KITAIFA

# Mwalimu mbaroni madai kukutwa na mwanafunzi

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

JESHI la Polisi mkoani Songwe, linamshikilia mwalimu wa Shule ya Sekondari ya Vwawa wilayani Mbozi, Paschal Vahaye (35), kwa madai ya kukutwa na mwanafunzi wa kidato cha sita nyumbani kwake akiwa uchi.

Inadaiwa mwanafunzi huyo (jina limehifadhiwa) anayeishi hosteli, alikwenda kwa mwalimu huyo kwa lengo la kufanya naye mpenzi.

Mwalimu huyo alikamatwa baada ya uongozi wa shule hiyo kuweka mtego kutokana na tuhuma za baadhi ya walimu katika shule huyo kudaiwa kujihusisha kimapenzi na wanafunzi wao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, George Kyando, alithibitisha kushikiliwa kwa mwalimu na kueleza kuwa tukio hilo lilitokea Novemba 28, mwaka huu, nyumbani kwa mwalimu mtaa wa Ilolo, mjini Vwawa, majira ya saa 4:30 usiku.

Alisema mwalimu huyo alikutwa akiwa na mwanafunzi huyo ambaye alikuwa uchi na kwamba anashikiliwa wakati uchunguzi unaendelea.

Akielezea tukio hilo, alisema mwalimu na mwanafunzi huyo walikamatwa kwa kushirikiana na uongozi wa serikali ya mtaa baada ya kupenyezewa taarifa na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi wanaohusika na idara ya elimu.

"Kimsingi tuliwakamata wote, lakini baadaye mwanafunzi tulimwachia kwa kumkabidhi kwa uongozi wa shule ili waendelee na taratibu zingine na tulifanya hivyo, ili kulinda usalama wa mwanafunzi maana baada ya tukio hilo, angeweza kuchanganyikiwa na baadaye kujidhuru.

"Lakini kwa upande wa mwalimu yeye ndiyo tunaendelea kumshikilia hadi uchunguzi utakapokamilika na hatimaye kumfikisha kwenye vyombo vya sheria," alisema.

Kamanda Kyando alisema uchunguzi wa awali uonaonyesha kuwa mwanafunzi huyo amekuwa na tabia ya kwenda mara kwa mara nyumbani kwa mwalimu huyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mbozi, Hanji Godigodi, alisema tukio la kukamatwa kwa mwalimu huyo ni sehemu ya mkakati wa kukomesha tatizo baada ya kupokea malalamiko mara kwa mara ya walimu kujihusisha kimapenzi na wanafunzi.

"Tumepokea malalamiko mara kwa mara, lakini ilikuwa vigumu kuchukua hatua bila kuwa na uthibitisho, hivyo kwa tukio hili ni wazi tutaenda kuchukua hatua kali sana ili iwe fundisho kwa wale wote ambao wanashindwa kuheshimu sheria na taratibu."



Wakulima wa Kijiji cha Rusoli, Musoma Vijijini, mkoani Mara, wakiandaa shamba lao juzi, kwa kutumia jembe la kukokotwa na ng'ombe (plau), ambalo kwa sasa hutumiwa na vikundi mbalimbali vya wakulima ikiwa ni mkakati wa kuachana na jembe la mkono. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakubaliana utekelezaji agizo la Rais

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI 10 za serikali zikiongozwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), zimekubaliana mambo ya msingi ya kutekeleza ili kuwezesha wawekezaji kupata vibali ndani ya siku saba hadi 14.

Makubaliano hayo yanakuja kutokana na agizo la Rais John Magufuli, alilolitoa wakati akizindua Bunge la 12 akiitaka TIC kuhakikisha inakamilisha vibali kwa wawekezaji wanaotaka kuwekeza nchini ndani ya siku 14.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana mara baada ya kikao kilichojumuisha wakuu wa taasisi hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Dk. Maduhu Kazi, alisema moja ya mambo hayo ni kutekeleza takwa la kisheria la kutoa vibali ndani ya siku 14.

Dk. Kazi alisema katika kuteleza hayo, wamekubaliana ndani ya siku saba hadi 14 kuhakikisha mwekezaji anakuwa amepata leseni, usajili na vibali vingine.

"Pia tumekubaliana taasisi zote zinazohusika kutokuwa na urasimu katika ofisi zetu ili kutimiza takwa hili la kisheria ambalo Rais ametukumbusha ili anapokuja mwekezaji nchini, anachotakiwa kuwaza yeye ni biashara tu na si kitu kingine," alisema Dk. Kazi

Vile vile alisema taasisi hizo zinatakiwa kuongeza matumizi ya mifumo mbalimbali inayotumia teknolojia ili kukamalisha shughuli mbalimbali za mahitaji ya wawekezajia kwa wakati.

"Katika kikao hiki pia tumeunda timu ya waataalam wetu wa mifumo ya kiteknolojia ambao watakutana muda si mrefu ili kuona ni njia gani tunaweza kuitumia ili kufanikisha utekelezaji maagizo haya ya Rais," alifafanua.

Dk. Kazi alisema jambo lingine walilokubaliana ni taasisi hizo kuhakikisha anapokuja mwekezaji anapatiwa maelekezo muhimu ya nyaraka zipi zinahaitaji ili kukamilisha mahitaji yake ndani ya siku 14.

"Shida iliyokuwapo awali ni kutokuwepo kwa ushirikanao baina ya taasisi hizi. Unakuta kuna mwekezaji anataka kuwekeza lakini taasisi nyingine hazina taarifa juu ya uwekezaji huo hali inayosababisha kuchelewesha baadhi ya michakato," alisema.

Kuhusu Kituo hicho kuhamia ofisi ya Rais, alisema kuwa hivi sasa bado wako katika kutayarisha miundo na itakapokamilika, watahamia rasmi.

Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Dk. Edwin Mhede, alisema kilichokuwapo awali ni matatizo ya kisheria lakini pia mtanzamo wa watendaji katika taasisi hizo.

Alisema hivi sasa watendaji katika taasisi hizo wanatakiwa kubadili mitazamo yao katika kufanikisha agizo la Rais la kukamilisha vibali vya wawekezaji ndani ya siku 14 na si vinginevyo.

Kamishna wa Ardhi, Matthew Nhonge, alisema watahakikisha maombi ya umilikishaji wa ardhi kwa wawekezaji yanatolewa ndani ya muda mfupi pamoja na kuboresha mifumo mbalimbali ya uombaji.


## BAM INTERNATIONAL BV TANZANIA
## DAR ES SALAAM

## MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na **BAM International Tanzania.** watauza kwa mnada wa hadhara Makontena matupu, Mitambo ya ujenzi na vifaa vya ujenzi tarehe 5 December, 2020 siku za Jumamosi saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika BAM International eneo la mradi Batching Plant (Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere) Terminal 3 Dar es salaam.

**VIFAA VYA UJENZI NA FANICHA ZA OFISI ZITAKAZOUZWA:**
Mobile Fencing, Manhole covers, Aluminum Profile, Galvanized street light poles, Steel and aluminum Scaffoldings, Podium Ladder, Pipe hard insulations, Mesh, Electrical items, Welding rods, Knauf Insulation materials, Sandwich panels, Fire Fighting fittings, Hose & Valves, Ceiling Tiles, Floor Tiles, Canon Photo Copy m/c C5235, Plotter HP 520,File Cabinets, Office Table, Chairs, Construction Plastic Spacers, Armoured Cables, Vyuma Chakavu na vingine vingi.

**MAKONTENA NA MITAMBO YA UJENZI YATAKAYOUZWA KUANZIA SAA 4:00 ASUBUHI**

| Idadi | Aina | Model | Hali yake | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 47 | Empty Container 40FT. | High Cub, STD& Open Top | Nzuri | Umelipwa |
| 8 | Pipe welding/Threading m/c | 160mm | Nzuri | Umelipwa |
| 4 | Welding m/c 250/ Inverter | 250 / 522 / 3 - Phase | Nzuri | Umelipwa |
| 1 | Table Saw machine | ZBV -450 | Nzuri | Umelipwa |
| 4 | Floor cutting machine | Honda | Nzuri | Umelipwa |
| 5 | Electric Concrete Poker Vibrator | LAIER | Nzuri | Umelipwa |
| 3 | Multi stage pump | 11Kw / 15 - HP | Nzuri | Umelipwa |
| 4 | Terrazzo Grinding machine | 3 phase | Nzuri | Umelipwa |
| 12 | Assorted Terrazzo Machine | Vacuum cleaner/ Polish | Nzuri | Umelipwa |

Mali zote zitakaguliwa **BAM International** eneo la mradi Batching Plant JNIA T3 Dar es Salaam, Tarehe 3 mpaka 4 December, 2020 kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 10:00 jioni

**MASHARTI YA MNADA:**
1. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi kabla ya December 11,020 saa 10:00 jioni kwenye bank Akaunti ya BAM utakayoelekezwa, ukishindwa kulipa kwa muda huo mali itauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
3. Mali iliyouzwa itatakiwa kuondolewa ndani ya siku 5 baada ya kulipa malipo yote.
4. Kila mtu atatakiwa kuwa na bid namba itakayo patikana getini.

**Kwa maelezo zaidi waone:**

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO. 5 "E" LION STREET SINZA**
**DAR ES SALAAM**
**CELL NO: 0754 284 926**
**E-mail: universalauction@hotmail.com**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bodi ya Mikopo itende haki dirisha la rufani

**JUZI** Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), ilitangaza awamu ya tatu ya wanufaika 3,544 wa mikopo ya Sh. bilioni 11.

Idadi hiyo inafanya jumla ya wanufaika kuwa 69,625 ambao wamepata kiasi cha Sh. bilioni 247.5 wanaendelea na masomo ambao wamefaulu kwa mwaka wa masomo 2019/2020.

Wanufaika 53,364 wa mwaka wa kwanza wamepangiwa mikopo ya Sh. bilioni 173.29, huku Bodi ikifungua milango la rufaa kwa siku saba kwa waombaji ambao wanaona kwa namna yoyote hawakuridhika na uamuzi uliotolewa.

Pia, Bodi hiyo imetoa wito kwa waombaji ambao hawajapangiwa mikopo na ni wahitaji kutumia muda wa siku saba za rufani kuwasilisha nyaraka sahihi ili hatimaye wapangiwe mikopo ya kuwawezesha kulipia gharama za masomo.

Tunapongeza jitihada ya kuhakikisha kuna wanufaika wengi wa mikopo hiyo, lakini bado wahitaji ni wengi na mara nyingi sifa zinawaangisha licha ya kuwa na viambatanisho vyote muhimu.

Tunatarajia kuwa siku saba za dirisha la rufani litatumiwa vizuri na waombaji na Bodi itahakikisha inapitia fomu moja baada ya nyingine ili kutenda haki kwa kila aliyekata rufaa kuonyesha kutoridhishwa na uamuzi wa kunyimwa mkopo.

Katika mitandao ya kijamii tumeona baadhi ya vijana wakieleza masikitiko yao ya kukosa mikopo kwa sababu alisoma shule nzuri za ada kubwa wakati wazazi wana uwezo, lakini katika safari ya maisha waliachishwa kazi, walifilisika, walistaafu na kufariki.

Kutokana na sababu hizo wameshindwa kuwalipia ada na mahitaji mengine ya chuo kikuu watoto wao na wengi kukimbilia Bodi, lakini nako wamekosa, hivyo kuzima ndoto zao za kusoma chuo kikuu.

Ni vyema suala hili likaangaliwa kwa kina na jicho la huruma; kwamba mwanafunzi ambaye mzazi wake alijitahidi kwa kipato alichokuwa nacho wakati huo, akahakikisha anamwekea msingi imara mwanaye kwenye elimu, sasa hana uwezo na ndiyo inakuwa mwisho wa safari ya mwanafunzi huyo kusoma chuo kikuu.

Ikiwa hivyo maana yake ndoto za mtoto huyo zinazikwa kwa muda mfupi, na kwa hali halisi ya soko la ajira, maana yake hatakuwa na ajira, hataweza kujiendeleza kwa kipato chake na wakati huo apambane na maisha katika kuwa na familia na kujenga maisha yake.

Ni ushauri wetu kuwa inapotokea kuna vielelezo vyote muhimu, ni vyema wanafunzi wapewe mikopo ambayo baada ya kuhitimu watakuwa na wajibu wa kuirejesha.

Wapo Watanzania wengi waliosoma hadi kidato cha sita, wana Diploma na sifa zote za kujiunga na chuo kikuu, lakini kutokana na uwezo mdogo wameshindwa kufikia ndoto zao na wako mtaani.

Katika utoaji wa mikopo hiyo waombaji hupata kwa viwango tofauti tofauti ambavyo kwa kiasi kikubwa huwapunguzia makali wazazi na walezi ambao uwezo wa kufanya kazi umepungua, kipato kimepungua na sababu nyingine nyingi.


Lakini ni muhimu sana kwa Bodi na serikali kwa ujumla kuangalia uwezekano wa kutoa mikopo kwa waombaji wote, ili waendelee na masomo yao, vinginevyo wapo ambao hawatafika chuo kikuu kutokana na ukata. Pamoja na jitihada za kuongeza idadi ya wanufaika kila mwaka, ni muhimu wanufaika wakaongezeka na kusiwe na vikwazo, na ikiwezekana walipiwe ada pekee, huku wazazi wakiwa na jukumu la kuhangaikia mahitaji mengine.

Wazazi kwa hiyari yao wanaona wanajiweza, ni vyema wakawasaidia watoto wao ili kutoa nafasi kwa wanafunzi wa familia zisizojiweza kupata fedha hizo ziwawezeshe kusoma.

Tunatambua kuwa urejeshaji wa mikopo nao una vikwazo vingi kiasi cha fedha nyingi kuwa nje kuliko inayopaswa kurejeshwa. Hii inatokana na wanufaika kupata mikopo na kuingia mitini, jambo ambalo linaumiza wengine.

Tunatambua kuwa upo mfumo mzuri wa ufuatiliaji wa madeni na wengi wanalipa ili kuongeza idadi ya wanufaika. Ni muhimu fedha hizo zikalipwa kwa wakati ili kuhakikisha mikopo inawafikia wengi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Choo ni kila kitu, ila ukweli wake kinavyohudumiwa bado ni mtihani

Na Halfani Chusi

**WATU** wanaojihusisha na masuala ya afya, wanakitaja kitengo muhimu katika nyumba kwamba ni choo. Katika matumizi ya kitengo hicho, kuna msisitizo wa namna ya kutumia unaoelekezwa katika usafi kiwango cha juu.

Ni dhana iliyopiga hatua ya mbali, kitaifa kuna kampeni inayoitwa 'nyumba ni choo.' Hapo maana yao ni kwamba, magonjwa mengi ya mlipuko kama vile kichocho, matatizo katika njia ya mkojo na mwili kupokea hewa chafu pindi mtu anapojisaidia, yote yanasababishwa na uchafu kutoka mazingira ya vyoo vichafu,

Licha ya wataalamu wa afya kuendelea kusisitiza hayo, bado hali ya vyoo iko vibaya na hasa katika nyumba za kupanga, maeneo ya jumuiya kama sokoni, shuleni viwanja vya michezo na nyumba za kulala wageni.

Katika baadhi ya sehemu hizo, inapochunguzwa kwa kina, inagundulika dhana ya choo haipewi kipaumbele cha kuwekwa safi, wakati ni kitengo muhimu kwa jamii husika.

Mara nyingi serikali imekuwa ikikagua nyumba zisizo na vyoo na kuchukuliwa hatua za kisheria, ikiwamo kuwapiga faini wahusika pale panapokutwa kuwapo ama hitilafu au kukosekana kabisa vyoo hivyo.

Mtazamo wangu raia na mkazi wa jumuiya ya Kitanzania, katika hili la namna gani vyoo vinafanya kazi yake, nashauri serikali za mitaa zilizoko katika himaya ya halmashauri mbalimbali nchini, kuna haja ya kuundwa mamlaka zinazofanana na kamati zitakazofanya kazi endelevu ya ukaguzi kati ya nyumba moja na nyingine.

Hapo, kuna mitazamo kama ubora wa vyoo na kutolewa maelekezo namna ya kiwango stahiki kinachopaswa kuwapo, ikiendana na ufuatiliaji wa kisheria wa utekelezaji ajenda, ili asiyefanikisha achukuliwe hatua.

Ukweli ulioko ni kwamba, kuna baadhi ya watu waliopanga katika nyumba mbalimbali, ambako anakutana na hali mbaya kiasi cha kutisha, mwenye nyumba hana mpango hata kidogo kufanya maboresho au kurekebisha mpaka, baadhi wakidiriki kutamka "kama unaona choo kibaya, hama au kajenge nyumba yako."

**Ukweli ulioko ni kwamba, kuna baadhi ya watu waliopanga katika nyumba mbalimbali, ambako anakutana na hali mbaya kiasi cha kutisha, mwenye nyumba hana mpango hata kidogo kufanya maboresho au kurekebisha mpaka, baadhi wakidiriki kutamka "kama unaona choo kibaya, hama au kajenge nyumba yako."**

Ndipo unakuta mpangaji anaendelea kudumu katika makazi hayo akiwa shingo upande, kwa sababu hana mbadala akiwaza itakapotokea anahama, ni wapi atapata penye choo kizuri?

Kwa kifupi, serikali na hasa ya mtaa inatakiwa kulijua hili na kuangalia namna ya kulisaidia kundi hilo kubwa la wapangaji, wanaoangukia vilio vya vyoo duni.

Hiyo ina maana kwamba, kuwafanya wenye nyumba ambao vyoo vyao havina ubora na wakati huohuo, hawana mpango wa kurekebisha, wanabadilika kwa lazima.

Ni shida inayopaswa kufanyiwa ukaguzi sokoni, shuleni, viwanja vya michezo, vituo vikubwa vya magari, hatua zitakazoisaidia jamii kuondokana na magonjwa yenye mzizi wa uchafu wa vyoo.

Hili lisiishie katika kauli yangu pekee, nilibahatika kuzungumza na kijana anayeishi nyumba ya kupanga na moja ya adha yake mahali hapo, ni choo.

Hapo ni eneo la Vingunguti, jijini Dar es Salaam, kunakojulikana kwa simulizi hiyo na kijana ana simulizi ya yanayomkuta, kwamba inafika hatua zenye kutia simanzi, mathalan uhalisia wa msalani, anayetaka kwenda chooni huko anafika hatua ya kughairi kujisaidia.

Ni mahali kunakokutwa kumesheheni uchafu kwa kiasi ambacho si staha ya kueleza. Utitiri wa wadudu ni mkubwa na inafikia hatua hapasafishiki na harufu kali iliyopitiliza.

■**Mwandishi anapatikana kwa namba +255 787879707.**




Ofisa Maji Bonde la Wami - Ruvu, Simon Ngonyani, akizungumza na waandishi wa habari, jana jijini Dar es Salaam, kuhusu utaratibu wa kufunga mita za maji katika viwanda vikubwa. Kushoto ni ofisa wa bonde hilo, Harold Kayoza. **PICHA: FRANK MONYO**

# China yaahidi kuendeleza utekelezaji miradi nchini

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI ya China imesema itaendelea kushirikiana na Tanzania katika shughuli na miradi mbalimbali ya maendeleo kama ambavyo imekuwa ikifanya.

Balozi wa China nchini, Wang Ke (pichani), alisema tangu kuanzishwa kwa Jukwaa la Ushirikiano kati ya China na Afrika (FACOC) miaka 20 iliyopita, kumechagiza kuboresha zaidi mahusiano katika nchi hizo.

Alisema mwaka huu wakati wakikumbuka kuanzishwa kwa ushirikiano huo wa FOCAC, watahakikisha wanaendelea kuboresha mifumo imara kwa ajili ya ustawi wa ushirikiano huo.

"FOCAC haijawahi kuwa si tu jukwaa la mazungumzo, bali limefanyika kama kikosi kazi ambacho hufanya mambo yatendeke kwa ubora zaidi, na katika kipindi cha miaka 20 iliyopita, imeunda na kutekeleza safu ya hatua zinazolenga kuleta matokeo mazuri, mipango na hatua zinazokidhi mahitaji ya China na Afrika, na kuleta faida zinazoonekana kwa pande zote hizo," alisema Ke.

"Mwaka 2019, uwekezaji wa moja kwa moja wa Wachina barani Afrika ulikuwa Dola za Marekani bilioni 49.1, ikiongezeka kwa karibu mara 100 kutoka mwaka 2000. Biashara ya China na Afrika ilifikia Dola za Marekani bilioni 208.7, na China imekuwa mshirika mkubwa wa



kibiashara barani Afrika kwa miaka 11 mfululizo, na imechangia zaidi ya asilimia 20 ya ukuaji wa bara hilo kwa miaka kadhaa."

"Miradi mingi ikiwa ni pamoja na reli, barabara, viwanja vya ndege, bandari za baharini na vituo vya umeme vimeanza kuzaa matunda barani humo. Kufikia sasa, China imetoa udhamini wa masomo 120,000 kwa watumishi wa serikalini kwa Afrika, na ilituma madaktari na wauguzi 21,000 katika timu za matibabu kwa mataifa 48 katika nchi hizo.

Alisema katika miaka hiyo 20, Tanzania imekuwa ikishiriki katika mikutano mbalimbali na pia kuchangia kikamilifu nguvu zake katika maendeleo kwenye jukwaa hilo la FOCAC.

"Mwaka 2018, Waziri Mkuu wa Tanzania, Kassim Majaliwa, akimwakilisha Rais John Magufuli, kwenye mkutano wa FOCAC Beijing, na alikutana na Rais wa China Xi Jinping. Viongozi hao wawili walifanya majadiliano ya kina juu ya maendeleo na uhusiano kati ya nchi hizo mbili," alisema Ke.

"Pia katika miaka 20, China na Tanzania zimedumisha mawasiliano ya kimkakati na kuimarisha ushirikiano wa faida kwenye jukwaa hilo na hivyo kuendelea kutoa msukumo mpya kwa ushirikiano katika maendeleo ya pande zote hizo mbili."

Alisema biashara na uwekezaji wa nchi hizo mbili kwa mwaka 2019 ilifikia Dola za Kimarekani bilioni 4.179, na kwamba nchi hiyo imekuwa mshirika mkubwa wa kibiashara wa Tanzania kwa miaka minne mfululizo.

"Uwekezaji wa moja kwa moja wa China nchini Tanzania ni zaidi ya dola za Kimarekani bilioni 7, na miradi zaidi ya 700 ya uwekezaji ikitoa karibu ajira 150,000 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa Watanzania. Biashara za Wachina zimeanzisha ustawi katika sekta kama vile mavazi, usindikaji wa bidhaa za kilimo na utengenezaji wa vifaa vya ujenzi," alisema Ke. Alisema uwekezaji huo umechangia utekelezaji wa mkakati wa kuhimiza vitu vya ndani kwa Tanzania katika maendeleo ya uchumi na mchakato wake wa viwanda.

# DC aagiza madanguro kufungwa

**Na Yasmine Protace,**
MKURANGA

MKUU wa Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, Ilbeto Sanga, ameviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuyafunga madanguro yote.

Amesema hatua hiyo itasaidia kupambana na kuwapo kwa maambikizi ya virusi vya Ukimwi (VVU).

Kufungwa kwa madanguro kutasaidia kuzuia kuenea kwa maambikizi ya VVU. Kwa sasa maambukizi ni asilimia 94 tofauti na matarajio ya wilaya ambapo matarajio yalikuwa asilimia 90.

Sanga aliyasema hayo juzi katika maadhimishoya Siku ya Ukimwi Duniani. "Madanguro lazima yafungwe ili kupunguza kasi ya maambikizi ya virusi," alisema.

Aliongeza kuwa uanzishwaji kwa madanguro kulichochea ongezeko la maambikizi mapya.

Akizungumzia matendo ya ulawiti, Sanga alisema ni jukumu la wazazi au walezi ni kujenga utamaduni wa kuwakagua watoto wao mara kwa mara pamoja na kuwafuatilia kwa karibu wanapokuwa wanacheza kwa kuwa kuna watoto wenye tabia ya kulawiti wenzao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga, Msham Munde, alizipongeza taasisi zisizo za kiserikali kwa kuendelea kuwasaidia watoto wenye uhitaji maalum kwa kuwapatia vifaa vya shule na bima za afya kwa kaya 896 zilizopo Mkuranga.

# Madaktari maalum watakiwa kushughulikia kesi za ubakaji

**Na Joseph Mwendapole**

BAADHI ya wadau wameshauri uwapo madaktari maalum wa kushughulikia kesi za ubakaji na ukatili wa kijinsia watakaopewa mafunzo na ulinzi, ili wawe huru kutoa ushahidi kwenye kesi hizo mahakamani.

Ushauri huo ulitolewa jana na washiriki wa kongamano ambalo ni mwendelezo wa siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia kuhusu namna ya kuwasaidia waathiriwa wa vitendo vya ukatili.

Kongamano hilo liliandaliwa na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) na kushirikisha maofisa kutoka Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali DPP, mahakimu wafawidhi, Jeshi la Polisi, madaktari na wadau wa taasisi zisizo za kiserikali (Ngo's).

Grolia Bartazari kutoka Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), alisema utaratibu wa sasa wa kila daktari kushughulikia mashauri ya ubakaji unasababisha kesi hizo kuchukua muda mrefu kumalizika kutokana na wengi kuzikacha.

Alisema ili kesi hizo ziwe nyepesi na zisikilizwe kwa haraka ni vyema wawepo madaktari watakaopewa mafunzo maalum kuhusu namna ya kujaza fomu namba tatu (PF3) na namna ya kutetea ushahidi wao wanapoitwa mahakamani.

"Madakatri hawa watawajibika kwa sababu hili ndilo litakuwa jukumu lao la msingi tofauti na sasa ambapo kila mtu anahusishwa, tukifanya hivyo tutasaidia hizi kesi ziishe haraka kwa sababu zikichelewa kunatoa mwanya wa uchakachuaji wa ushahidi," alisema Grolia.

Mshiriki mwingine, Selemani Yusuf, aliunga mkono hoja hiyo, akisema kuwa baadhi ya madaktari wanakimbia kesi za ubakaji kutokana na kuchukua muda mrefu kusikilizwa. Alisema kuahirishwa kwa kesi mara kwa mara kumekuwa kukiwachosha madaktari wanapoitwa kwenda kutoa ushahidi wao kuhusu vipimo walivyofanya kwa muathiriwa.

"Unakuta daktari anaitwa mahakamani anaenda asubuhi, lakini mpaka saa nane kesi haijaanza na mwishowe anaambiwa kwamba kesi imeahirishwa sasa ndiyo sababu wengi hawataki kabisa kuona PF3," alisema. Dk. Rahina Ali wa Kituo cha Afya Kigamboni, alisema madaktari wengi hawapendi kuhudumia wagonjwa wanaokwenda na PF3 kwa hofu ya usumbufu watakaoupata wa kwenda kutoa ushahidi wao mahakamani.

"Kwanza hatuna ulinzi, sisi ni tofauti kabisa na polisi kwa sababu wao angalau wanaogopwa na wengine wana silaha sasa sisi madaktari tuna sindano tu, hivyo kuna haja ya kuwawekea mazingira mazuri madaktari," alishauri.

Gema Akilimali, mwanachama wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), alishauri kesi za ukatili wa kijinsia ikiwamo ubakaji zipewe kipaumbele ili zikamilike kwa wakati. Alisema kama polisi wanakerwa na vitendo vya ukatili wa kijinsia basi wanapaswa kuharakisha kukamilisha ushahidi wa kesi hizo, ili wahusika wachukuliwe hatua.

# Mkandarasi, mshauri walipa mil. 1.3/- kwa kukiri kutoa rushwa

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Geita imewahukumu mkandarasi na mhandisi mshauri kutumikia kifungo cha miaka miwili jela au kulipa faini ya Sh. 1,300,000 kwa kosa la kushawishi na kutoa rushwa ya Sh. milioni 10.

Washtakiwa hao ni Yassin Ally (49) ambaye ni mkandarasi na mkazi wa Kasulu mkoani Kigoma na Alexander Lufunga (62) mhandisi mshauri na mkazi wa Mbezi Beach, Dar es Salaam.

Ally na Lufunga walipatikana na hatia ya kutoa fedha hizo kwa Mgasa Justin na Juma Musa, ambao ni watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale ili wapewe upendeleo wa zabuni ya kusambaza mabomba ya maji yenye thamani ya Sh. milioni 410 ambazo alichukua mshtakwa Ally na hakufanya kazi iliyokusudia, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria.

Hata hivyo, washtakiwa hao walikiri makosa na kulipa faini kisha waliachiwa huru. Hukumu hiyo imetolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Samuel Maweda. Hakimu Maweda alisema washtakiwa wote wawili waliposomewa shtaka lao walikiri kosa na pia wameirahisishia mahakama kwa upotevu wa muda, hivyo basi mahakama inawahukumu kwenda jela miaka miwili au kulipa faini ya Sh. 1,300,000 wote wawili. Pia hakimu alimwamuru Ally kurejesha serikalini Sh. milioni 410 ndani ya miezi 18 na akishindwa, mali zake zitataifishwa ili kufidia kiasi hicho cha fedha.

Akisoma hati ya mashtaka jana, Wakili Kiongozi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Geita, Kelvin Murusuri, alidai kuwa kati ya Januari Mosi na Mei 3, 2014 katika Wilaya ya Nyang'hwale, washtakiwa wakiwa mkandarasi na mwenzake mshauri katika mradi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyanghwale, wakiwa wasambazaji wa mradi wa maji katika vijiji vya Kakora na Nyarubele, walitoa rushwa ya Sh. milioni 10 kwa Mgasa Jastini na Juma Musa.

Lengo la kutoa rushwa hiyo, kwa mujibu wa Murusuri, ni kupata upendeleo wa tenda ya kusambaza mabomba ya maji yenye thamani ya Sh. milioni 410.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikabidhi tuzo kwa Kaimu Ofisa wa Fedha Mkuu wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa (kushoto), kwa kutambua mchango wa benki hiyo, kudhamini kongamano la 11 la wataalamu wa manunuzi na ugavi (PSPTB), jijini Arusha jana. Wa (pili kulia) ni Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango na Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waonywa uwekaji gharama kubwa

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

MAKANDARASI wametakiwa kuwa waaminifu wanapoomba zabuni badala ya kuweka bei kubwa isiyolingana na mradi wanaoomba kuutekeleza.

Hayo yalisemwa jana mjini hapa na Mwenyekiti wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), Consolatha Ngimbwa, wakati wa mkutano wa siku tatu kwa makandarasi wa Nyanda za Juu Kusini, unaofanyika mjini hapa.

Alisema vitendo vya baadhi yao kutokuwa waaminifu, vimesababisha serikali kupoteza imani nao, hivyo kutumia mfumo wa 'force account' wa kutekeleza miradi yake ya ujenzi yenyewe badala ya kutumia makandarasi.

Ngimbwa alisema baadhi ya michakato ya zabuni za ununuzi wa umma, ikiwamo ujenzi wa miundombinu, imegubikwa na viashiria vya rushwa, hivyo kuwafanya makandarasi kutia saini mikataba bila kuisoma vizuri.

"Baadhi ya makandarasi si waaminifu na wamesababisha serikali kupoteza imani nao, hivyo kutekeleza miradi bila kutumia makandarasi," alisema.

Pia alisema ushindani katika kupata zabuni umekuwa mkubwa tofauti na miaka mitano iliyopita, hivyo utaalamu wa kutosha unahitajika kwa makandarasi katika kujaza zabuni na ikakubalika.

Aliwataka makandarasi kuwa wakweli, wawazi, wazalendo na kujiepusha na vitendo vya rushwa wakati wa kutekeleza miradi ya ujenzi ili kufanya kazi bora zitakazowajengea imani kubwa.

Sambamba na hilo, aliwataka makandarasi kujiunga katika chama kimoja ambacho kitakuwa imara ili iwe rahisi kwa kudai haki zao pale ambapo watahitajika kufanya hivyo.

Msajili Msaidizi wa CRB, Mhandisi David Jere, alisema mafunzo hayo yatawasaidia makandarasi namna ya kujenga bei ya makisio ya zabuni ambayo mara kadha imekuwa ikilalamikiwa na waajiri.

"Wakati mwingine makandarasi wetu wamekuwa wakiweka bei ambayo si halisi sambamba na hilo tutafanya mafunzo ya mfumo wa kieletroniki wa manunuzi ya umma," alisema Jere.

Baadhi ya makandarasi kutoka mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, wakiwamo Edgar Mtitu na Charles Mhagama, walisema mafunzo hayo yana tija kwao hasa kwa makandarasi vijana kuwa yatawajenga kikamilifu kwenye shughuli zao za kikazi.

"Ameonyesha njia na amesisitiza sisi vijana tunatakiwa tuonyeshe mfano, hivyo sisi kama vijana makandarasi, tunatakiwa tutumie ushauri wake kama fursa kuonyesha mfano huo," alisema Mtitu.

Mhagama alisema kuwa mara nyingi wanapopata kazi huwa wanakwenda kutia saini mikataba na sehemu kubwa baadhi yao huwa hawapitii mikataba hiyo.

"Sasa tumekumbushwa namna sahihi ya kupitia mikataba na ikibidi kupata mshauri ambaye atakusaidia namna ya kusoma mkataba huo," alisema Mhagama.

## Equity Bank yazindua kadi ya kisasa Dola

**Na Gwamaka Alipipi**

TAASISI inayotoa huduma za kifedha, Equity Bank Limited, imezindua kadi mpya ya kisasa ya visa inayotumia mfumo wa sarafu ya Dola ya Kimarekani, kwa ajili ya matumizi ya wateja wake hapa nchini.

Kadi hiyo iliyotengenezwa kwa kiwango cha dhahabu ni ya kwanza na ya kipekee ikiwa na malengo ya kutoa urahisi na upatikanaji wa huduma kwa wateja wa benki hiyo, ambao wanataka kufanya manunuzi kupitia mtandaoni au kufanya biashara kwa kutumia sarafu ya Dola ya Kimarekani.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kadi hiyo, jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Robert Kiboti, alisema kadi hiyo ni nafuu, inatoa suluhisho la bei, ni rahisi na salama kwa mteja.

Alisema pia itamsaidia mteja katika kurahisisha huduma kwa wakati sahihi, lakini kuchochea ukuaji wa biashara ya mtandaoni.

Kiboti alisema kadi hiyo inampa mteja fursa ya kulipia bidhaa na huduma mbalimbali kwa sarafu ya Dola ya Kimarekani pasipo na nyongeza ya malipo yoyote ya ziada. Itamsaidia mteja kufanya miamala pasipo kuvuruga bajeti yake.

"Kadi ya Visa Gold Debit inaruhusu wateja kulipia bidhaa au huduma kwa Dola za Kimarekani kwa viwango vilivyoonyeshwa kwa wakati huo.

Hii inamaanisha kuwa ikiwa unalipa bidhaa inayouzwa Dola 10 za Kimarekani, hiyo ndiyo inayokatwa katika akaunti yako, hakuna malipo mengine," alisema Kiboti.

Alisema Visa PayWave ni teknolojia ya malipo isiyohusisha mawasiliano ya moja kwa moja, isipokuwa kupitia mawasiliano ya kimtandao kwa kutumia chipu maalumu.

Kiboti alisema: "Kadi hii inatumia mfumo wa chip na neno la siri kwa ajili ya usalama na ubora kwa mtumiaji."

Uzinduzi huo unakuja kufuatia mwenendo wa mabadiliko ya biashara ya kielektroniki, wakati ambao biashara nyingi zinahamia katika mtandao, ikiwa ni mojawapo ya madhara ya mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona.

HABARI KITAIFA

# Kasi maambukizi VVU Pwani yamshtua RC

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, ameshtushwa na taarifa za maambukizi ya virusi vya Ukimwi katika Halmashauri za Mji Kibaha, Chalinze na Mkuranga.

Kutokana na takwimu hizo, amewataka viongozi wa halmashauri hizo kuandaa mikakati ya kudhibiti maambukizi mapya ya VVU, ili kupunguza kasi hiyo.

Ndikilo alisema hayo juzi mjini hapa wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani ambayo kimkoa yalifanyika Bagamoyo, huku ikibainishwa kuwa halmashauri hizo zimeeleza kuongoza kwa maambukizi mapya ya VVU, huku chanzo kikielezwa kuwa ni mwingiliano wa shughuli za kiuchumi.

Alisema takwimu za maambukizi kwa mkoa huo za mwaka 2012 ni asilimia 5.9 na kwamba kilishuka hadi asilimia 5.5 kwa mwaka 2017.

Pamoja na kushuka kwa maambukizi, alisema bado halmashauri hizo zinaonekana kuwa na maambukizi mengi sababu sikielezwa kuwa biashara, viwanda vingi na vituo vya magari makubwa.

Hata hivyo, maambukizi kwa wanawake kuanzia Januari hadi Novemba, mwaka huu, maambukizi yanaelezwa kufikia asilimia 4.3 huku kwa wanaume yakiwa asilimia 3.6.

"Pamoja na takwimu hizi suala la upimaji wa hiari idadi kubwa ya wanaopimwa wanaelezwa kuwa ni wanawake kulinganisha na wanaume. Imeelezwa kuwa wanaume wanaonekana kuwa waoga," alisema.

Ndikilo alisema moja ya vikwazo vinavyoelezwa kuchochea maambukizi mapya ni pamoja na mila potofu, ndoa za ututoni na ngoma za usiku.

Katibu Tawala Mkoa wa Pwani, Delphine Magere, aliwataka wanawake kuwa wa kwanza kupinga maambukizi mapya kutokana na umuhimu wao kwenye majukumu ya kifamilia.

Akisoma risala ya watu wanaoishi na VVU, Elizabeth Hassan, alisema kikwazo kilichopo katika kundi hilo ni baadhi ya watu wanaoishi na virusi hivyo ni kusitisha kutumia dawa za kurefusha maisha (ARV).



Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, mkoani Shinyanga, Timoth Ndanya, akimpatia dawa ya minyoo mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika kimkoa katika Kata ya Mapamba, Halmashauri ya Ushetu, juzi. Kushoto ni Mratibu wa Afya ya Uzazi Mama na Mtoto, Dina Kamata. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Mchakato kumpata meya wakwama tena

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeshindwa kumpata mgombea umeya katika Manispaa ya Morogoro baada ya wanachama wake wawili walioteuliwa kuwania nafasi hiyo, kufungana kwa kura mara tatu.

Wagombea hao walifungana kwa kupata kura 21 kila mmoja katika mchakato wa marudio baada ya matokeo ya awali kutenguliwa.

Mchakato huo wa marudio, uliwashirikisha Mhandisi Hamis Ndwata aliyepata kura moja, meya wa zamani anayetetea nafasi hiyo, Paschal Kihanga kura 20 na Diwani wa Mkundi, Seif Chomoka akipata kura 21.

Kwa kuwa kanuni zinataka mshindi awe na zaidi ya nusu ya kura, ililazimika uchaguzi huo kurudiwa kati ya Chomoka na Kihanga. Katika mara zote tatu, kila mmoja alipata kura 21, hivyo kutokana mtu wa kupeperusha bendera katika uchaguzi wa Meya.

Msimamizi wa uchaguzi huo, ambaye ni Katibu wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Salum Khatib Teja, alisema kwa kuwa mshindi hajapatikana, atawasilisha uamuzi huo kwa Kamati ya Siasa ya Mkoa, ili waishauri Kamati Kuu ya CCM kuhusiana na kilichoendelea.

Mmoja wa wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Mkoa wa Morogoro, Vitus Lipagila, alisema mchuano huo unaonyesha wanachama hao wanakubalika, hivyo kuwataka madiwani kuwa wavumilivu na waridhike na matokeo yoyote ya kumpata atakayerejeshwa kugombea umeya na kuiendesha manispaa hiyo.

Kaimu Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Morogoro, Hassan Bantu, aliwahimiza madiwani hao kurudi kufanya kazi za maendeleo za kuwatumia wananchi pindi watakapompata meya.

Bantu akawataka madiwani kumpa ushirikiano meya atakayechaguliwa ili kutimiza wajibu wao wa kupeleka maendeleo kwa wananchi.

Kihanga na Chomoka, wakizungumzia walivyopokea uamuzi huo, kwa nyakati tofauti walisema wana imani na vikao vitakavyokwenda kufikia uamuzi na wako tayari kwa uamuzi wowote utakaofikiwa.

Uchaguzi wa awali wa kupata mgombea umeya wa Manispaa ya Morogoro, ulifanyika Novemba 23, mwaka huu. Chomoka aliongoza na kutangazwa mshindi kwa kupata kura 20, huku Kihanga na Ndwata wakipata kura 11 kila mmoja.

Hata hivyo, Kihanga alikata rufani kwa madai kuwa kanuni za kumpata mshindi zilikiukwa kwa vile mshindi hakupata zaidi ya nusu ya kura, hivyo CCM kuamuru kurudiwa upya.

## Bonde la Wami sasa kufunga mita za maji kwa watumiaji

**Na Frank Monyo**

BODI ya Maji Bonde la Wami – Ruvu (WRBWB), imesema ifikapo Februari, mwakani, itakamilisha kufunga mita za maji katika viwanda vyote vinavyotumia maji kutoka bonde hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Saalam, Mkurugenzi wa WRBWB, Simon Ngonyani, alisema wamekubaliana na Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania (CTI), kampuni na taasisi mbalimbali kufunga mita hizo katika viwanda vyao, ili kupata kiwango sahihi cha maji wanayotumia ili kulipa ada ya matumizi stahiki.

Alisema kumekuwa na udanganyifu kwa baadhi ya wamiliki wa viwanda kulipa ada ya matumizi ya maji tofauti na viwango wanavyotumia, na hivyo kusababisha usumbufu na kukwamisha juhudi za utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji.

Alisema kuwa hivi sasa matumizi ya maji yamekuwa yakiongezeka huku ikizingatiwa maana maji yanayotumika kwa sasa ni yale yale yaliotumiwa na zamani.

"Maji tunayotumia kizazi chetu ni yale yale yaliotumiwa na wazee, sasa hii ina maana kuwa ongezeko la shughuli za kibinadamu, mabadiliko ya tabia nchi yanapelekea vyanzo vya maji kuwa hatarini kupungua hivyo WRBWB imelazimika kuleta mbadala wa shughuli za kibinadamu ambazo haziathiri vyanzo vya maji," alisema Ngonyani.

Aidha, alisema maji yasipotunzwa yatakwisha, na kwamba hatua zinapaswa kuchukuliwa.

"Nawashukuru sana wenzetu wa CTI wamekuwa wakitoa ushirikiano, imefika mahala wametambua ni lazima walipe ada ya matumizi ya maji na sio kwamba hizo ada tunalipana mishahara, hapana; pesa hizo inakwenda kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji," alisema.

Alisema kuwa zipo shughuli mbalimbali zinazofanywa kupitia ada ya watumia maji, ikiwamo kupanda miti katika vyanzo vya maji na kujenga lambo kwa ajili ya manywesheo ya mifugo.

Alisisitiza kuwa kifungu hicho kinamtaka mtu yoyote anayetaka kuchepusha, kukinga, kuhifadhi, kuchukua na kutumia maji kutoka kwenye chanzo cha maji juu ya ardhi au chini ya ardhi au kujenga miundombinu yoyote lazima aombe kibali cha kumia maji.

HABARI KITAIFA

# NCC yafikisha elimu ya Ukimwi kwa wafanyakazi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI dunia ikiadhimisha Siku ya Ukimwi, Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC), limesema limefikia malengo yake ya kuhakikisha wafanyakazi wanaelimishwa kuhusu ugonjwa huo na maambukizi ya virusi visababishavyo ugonjwa huo, kwa mwaka huu.

Pia, limesema litahakikisha zana muhimu zinazohitajiwa na wafanyakazi kwa ajili ya kujikinga na maambukizi ya VVU na Ukimwi (kondomu) zinaendelea kupatikana kwa urahisi katika maeneo yote ambako zinapaswa kuwapo ndani ya ofisi hiyo, kwa ajili ya wahusika kuchukua na kwenda kuzitumia wanapokuwa wakizihitaji.

Mtendaji Mkuu wa Baraza hilo, Dk. Matiko Mturi, alisema hayo jijini Dar es Salaam juzi kuwa, mpango wa kulinda wafanyakazi wake dhidi ya maambukizi ya magonjwa hasa Ukimwi ni endelevu na kwamba unatekelezwa kupitia mafunzo, ushauri nasaha na njia nyingine zinazotumika kufikisha ujumbe kwa wafanyakazi kuhusu namna bora ya kujikinga, kama vile semina na maandiko mbalimbali vikiwamo vipeperushi na ajenda maalumu kwenye vikao vyote vya wafanyakazi.

"Tunashukuru kwamba wafanyakazi wa NCC wamekuwa wakitoa ushirikiano wa hali ya juu kufanikisha utekelezaji wa mpango mkakati wetu wa kuwapa elimu kuhusu masuala ya afya hususan namna ya kujikinga na maambukizi ya VVU pamoja na mambo yote wanayopaswa kuyajua kuhusu Ukimwi," alisema.

Kutokana na maelezo ya Dk. Mturi, NCC ilifanikiwa kupima kwa hiari wafanyakazi wake, baada ya kuwaandaa kisaikolojia na kufanikiwa kuwapa elimu iliyohitaji si tu kuhusu Ukimwi bali hata magonjwa mengine ambayo walipaswa kupata elimu kuyahusu.

Alisema lengo la kuweka mpango mkakati huo, pamoja na kutimizwa kwa matakwa ya serikali ya kuhakikisha vita dhidi ya maambukizi ya VVU na Ukimwi vinapiganwa hata katika maeneo ya kazi kwa wafanyakazi kupewa elimu ya kujikinga na maradhi, ni kuhakikisha usalama wa afya za wafanyakazi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

"NCC inajali na kuthamini afya ya wafanyakazi wake, kwa sababu ndio watenda kazi wanaotegemewa katika uzalishaji wa kila siku, hivyo kutokuwa na afya njema kwao ni tatizo pia kwa mlolongo mzima wa utendaji katika baraza."

"...Tunaendelea na tutaendelea kuhakikisha elimu zaidi inatolewa kwa wafanyakazi wote ili wajue namna bora ya kujilinda na kulinda wanajamii wengine wanaowazunguka dhidi ya magonjwa kama vile Ukimwi na mengine yanayoambukiza," alisema.



Mwanasheria kutoka Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Beatrice Mpembo (kulia), akizungumza wakati wa mjadala kuhusu namna ya kuwasaidia waathiriwa wa matatizo ya vitendo vya ukatili wa kijinsia, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Mkurugenzi wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo (WiLDAF), Anna Kulaya na Hakimu Mfadhidhi Mahakama ya Ilala, Martha Mpanze. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# StamiGold yalia gharama uzalishaji dhahabu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KAMPUNI ya uchimbaji dhahabu ya StamiGold, imelalamikia gharama kubwa za uzalishaji wa madini hayo.

Meneja wa kampuni hiyo yenye mgodi wake katika wilaya ya Biharamulo, Mhandisi Gilay Shamika, alibainisha hayo kwenye kilele cha Maonyesho ya Biashara na Teknolojia ya Madini mjini hapa.

Alisema mgodi huo tangu uwe chini ya serikali mwaka 2014 na kuanza uzalishaji rasmi mwaka 2017, umekuwa ukiingia kwenye gharama kubwa ya uzalishaji kutokana na kutumia jenereta. "Tunaiomba serikali ituunganishie huduma ya umeme kwenye mgodi huu, ili tupunguze gharama kubwa ya uzalishaji dhahabu kwa sababu kwa sasa tunatumia jenereta na mafuta ya dizeli," alisema. Alitaja gharama ambazo wanazitumia kwa mwezi kuzalisha dhahabu kutokana na kutumia jenereta kuwa ni Sh. bilioni 1.2 na kubainisha endapo wakitumia umeme itawagharimu Sh. milioni 300.

Mwenyekiti wa Tume ya Madini, Prof. Idris Kikula, akiwa kwenye banda la StamiGold, alipongeza mgodi huo kwa kufufuka tena na kuanza uzalishaji.

Prof. Kikula alilitaka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kuongeza wigo wa utoaji wa huduma ya umeme kwenye makazi ya watu, ikiwamo na maeneo ya migodi.

Pia alizitaka taasisi za kifedha kuweka mfumo kwa ajili ya kuwakopesha wachimbaji wadogo ili wapate mitaji kwa ajili ya kununua mitambo mikubwa ya uchimbaji wa madini na kufanya uzalishaji mkubwa.

# RUWASA, DataVision kufanya utafiti vituo maji vijijini

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa kushirikiana na DataVision International, wanatekeleza mradi wa Malipo kwa Matokeo (PBR) awamu ya tano, ukiwa na lengo la kufanya utafiti na ukaguzi wa vituo vya maji vijijini ili kuongeza upatikanaji wa huduma hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa mafunzo ya ukusanyaji takwimu za mradi huo unaofadhiliwa na Serikali ya Uingereza yaliyoendeshwa na DataVision International jijini Dar es Salaam, Meneja Takwimu wa RUWASA, Singolile Mwamwaja, alisema mradi huu ulianza mwaka 2016 na sasa uko katika awamu ya tano ukilenga kuzinufaisha halmashauri 179. "Tulianza awamu ya kwanza mwaka 2016 tukiwa na idadi ya halmashauri 57 zilizofanikiwa, awamu ya pili kulikuwa na halmashauri 92, awamu ya tatu halmashauri 181, kadhalika awamu ya nne halmashauri 181 na sasa awamu ya tano kuna halmashauri 179," alisema.

Alisema mradi huo utaongeza kiwango cha fedha za kuendeleza miundombinu katika halmashauri na kuwafikishia watu wengi zaidi huduma ya majisafi, kwani utafiti utakaolenga kutambua vituo vya maji vinavyofanya kazi kwa kutoa majisafi na salama na kama miundombinu ya vituo hivyo iko kwenye hali ya ubora, utaziwezesha halmashauri kupewa pauni 300 (Sh. 925,000) kwa kila kituo cha maji kitakachokuwa kinafanya kazi. Kupitia mradi huo kwa mwaka huu, vijiji 1,058 vimechaguliwa na vituo 1,695 vitapitiwa, kwa mujibu wa RUWASA.

"Matarajio yetu kwanza ni kuongeza kiwango cha fedha ambacho kinapatikana katika kila halmashauri, kwa sababu katika mradi kama kituo kinafanya kazi kinalipwa Pauni 300, na kiwango hicho cha fedha kinasaidia kuinua miundombinu na kuwafikia watu wengi zaidi, kwa sababu idadi ya Watanzania wanaoishi vijijini inazidi kuongezeka kila siku na huduma ya maji bado haijafika sehemu zote," aliongeza.

Meneja huyo alisema kama Rais John Magufuli alivyoeleza dhamira ya kuongeza huduma ya majisafi na salama ambayo hadi sasa imefikia asilimia 70.1, mpango wa serikali ni kufikia asilimia 90 ifikapo mwaka 2025. Alisema wakati unaanza kulikuwa na vituo takribani 87,000, lakini kupitia mradi huo sasa kuna vituo vya maji takribani 154,000.

Naye Sharif Nassor, Msaidizi wa Takwimu wa DataVision International, alisema kampuni hiyo ya kizalendo ambayo ni washindi wa tuzo ya kampuni bora zaidi katika utoaji wa huduma za utafiti, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) mwaka 2019 (East Africa Brand Leadership 2019), wametoa mafunzo ya ukusanyaji taarifa na watafanya kazi hiyo katika halmashauri zote 179.

"CDMT wanatuwezesha sisi kufahamu vile vyanzo vya maji vinavyopatikana kwenye mikoa yote 26 Tanzania, sisi tunahakiki ufanyaji kazi wa vituo husika," alisema Nassor na kuongeza kuwa tayari timu itakayokusanya takwimu imepewa mafunzo maalum kwa ajili ya kufanya kazi ya kukusanya taarifa kwa ufanisi na kwa kutumia teknolojia ya simu.

ALHAMISI DESEMBA 3, 2020
AFYA NA MAZINGIRA





Ukurasa 13

Shinyanga inavyochechemea ndani ya tope zito la utapiamlo sugu kwenye mkoa




Ukurasa 14

Pwani katika vikumbo kujichomoa utapiamlo

AFYA

# Kangaroo; mbinu inayofuta robo vifo vya njiti walioko hospitalini

• Mzaliwa hali hiyo ajitosa kuwapigania

**Na Christina Mwakangale**

KUZALIWA njiti, haiegemei historia ya mama kutoka familia duni au la. Inatokea pale kunapokuwapo hitilafu yeyote wakati wa ujauzito.

Kimataifa, Tanzania inashika nafasi ya 20 kwa kuwa na watoto wengi wanaozaliwa njiti, jumla yao wako 213,000 kila mwaka na kati yao njiti 40,000 wanafariki ndani ya kipindi hicho kutokana na matatizo mbalimbali, ikiwamo upumuaji duni.

Pia, ni kati ya nchi 10 duniani zinazochangia asilimia 66 ya vifo vya watoto wachanga, kutokana na matatizo mbalimbali ikiwamo uzito mdogo. Kwa mujibu wa wataalamu wa afya mimba huchukua wiki 38 hadi 42 mtoto kuzaliwa.

Kangaroo ni mtindo unaotumiwa na kitengo cha kulea watoto njiti kilichopo Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kwa kuiga namna ya malezi ya mnyama aitwaye Kangaroo, anayemhifadhi mtoto wake katika mfuko wa asili uliopo nje ya tumbo na kumfanya mtoto kupata joto muda wote.

Mtoto anayezaliwa chini ya miezi tisa na uzito mdogo, kiafya anapaswa kutumia kangaroo nyumbani au akiwa hospitalini na kuwekewa vifaa vya upumuaji.

Mganga Bingwa wa Watoto na Watoto Wachanga hadi vijana umri miaka 28, kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Augustine



Dk. Deborah Maufi, mdau katika vita vya kuokoa watoto njiti.



Doris Mollel; alizaliwa mapacha njiti, leo yuko mstari wa mbele vitani kuwaokoa. **PICHA ZOTE: CHRISTINA MWAKANGALE**

Massawe, ameiambia Nipashe kwamba utafiti uliofanywa mapema mwaka huu na hospitali hiyo, umeonyesha kangaroo imepunguza vifo vya watoto njiti kwa asilimia 25.

**MBINU ZA KUWAOKOA**

Anasema utafiti huo, MNH kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani (WHO) kwenye nchi tano ikiwamo Tanzania, Ghana, Malawi, Nigeria na India, umebaini mtindo huo utaokoa vifo vya watoto hao kwa nchi zinazoendelea, ambazo kwa kiasi kikubwa hushindwa kumudu gharama za matibabu, vifaa vya kuhudumia kabla ya uzazi, ikiwamo anachokiita 'incubators' katika kila hospitali nchini.

Dk. Massawe anataja vifaa vingine, ni mipira ya kupumua, hewa ya oksijeni, dawa za kukomaza mapafu na kwamba njia ya kangaroo haina gharama.

Kwa sababu mama mwenye mtoto njiti, anatajwa kuwa na uwezo wa kutumia nguo za asili, kikiwamo kitenge kwa kumbeba mtoto wake na kumpa joto.

"Niliandika 'proposal' (hoja) hapa MNH na kusimamia hii study (mapitio kitaalamu) iliyomalizika Februari mwaka huu, katika nchi hizo tano pamoja na WHO.

"Tunafuatilia watoto walioingia katika utafiti huu, kwamba Kangaroo inasaidiaje. Zamani ilikuwa unangoja mtoto awe 'stable' (amekoma) ndio umpeleke kwa mama yake.

"Hivi sasa hata kama anahema kwa shida, anakaa na mama yake akimbeba kwa mtindo wa kangaroo, tunataka hadithi ya theluthi moja ya watoto wanazaliwa njiti. Tunahitaji sehemu ya kutunza watoto iwe kila hospitali. Mkoa wa Dar es Salaam wanazaliwa watoto njiti 2,000," anasema.

Massawe, anasema kwa miaka miwili iliyopita, MNH ilifanya utafiti na ilionekana njia hii ni nzuri na njia hiyo ya mama kubeba mtoto 'ngozi kwa ngozi' hata kama mtoto atahitaji oksijeni, imetafitiwa ikaonekana asilimia 25 ya watoto hawa 'wamesurvive' (wamesalimika) kutokana na nyenzo kangaroo.

**SABABU NJITI**

Dk. Massawe anataja kuwapo mengi yanayosababisha mtoto kuzaliwa kabla ya muda, ikiwamo mjamzito kuugua maradhi kama malaria, presha, kifua kikuu na mkojo mchafu 'UTI', kisukari, upun-

INAENDELEA UK.12

AFYA

# Kangaroo; mbinu inayofuta robo vifo vya njiti walioko hospitalini

INATOKA UK.11

gufu wa damu (anemia), mapacha, uzazi wa mapema na lishe duni.

Aidha, zipo ambazo kitaalamu sababu zake inashinidikana kujulikana sababu za mtoto kutoka tumboni mapema kabla ya muda.

"Nchini Tanzania, kinamama wengi wanazaa watoto wenye kilogramu tatu, wakiwa na wiki 38 ya mimba," anasema Dk. Massawe na kuongeza:

"Akizaliwa wiki 28 ujue mtoto atakuwa na kilogramu moja. Hii ni hatari, angalau awe amezaliwa hospitali ambako 'wata-treat' (kumshughulikia) vizuri. Akizaliwa nyumbani, akipata baridi anafariki."

**DARASA UGHAIBUNI**

Dk. Deborah Maufi, Mwakilishi wa asasi Babymoon ya Uholanzi, inayohusika na utengenezaji bidhaa za kubeba watoto njiti kwa kutumia mtindo kangaroo, anasema kunahitajika elimu ya awali kujiandaa na kujifungua kwa kinamama walezi wa kangaroo, tangu zama za ujauzito.

"Kwa tofauti niliyoiona kwa nchi ya Tanzania na Afrika kwa ujumla, ni elimu kuhusu utunzaji watoto njiti. Wenzetu elimu ya watoto hawa hutolewa mapema tangu mama akiwa mjamzito kliniki.

"Huku hadi mama ajifungue ndio atapewa elimu. Elimu itolewe kwa kila mama sababu huwezi jua atajifungua mtoto njiti au la," anaeleza.

Dk. Deborah anabainisha katika nchi zilizoendelea, kuna vifaa maalum vya kutunza watoto hao, vikiwamo vya kuwapa joto na hewa na oksijeni, hitaji lenye upungufu kwenye nchi zinazoendelea zina uhaba wa vifaa hivyo.

"Vitu ambavyo tunaweza kutumia kwa huku Afrika tuna khanga kwa kubebea watoto. Ubebaji huu una matokeo chanya, ingawa awali tulikuwa tunachukulia 'poa.' Inasaidia sana mama akimbeba njiti 'ngozi kwa ngozi katika ukuaji

Anasema, alianza kufanya kazi hiyo baada ya kukutana na mwanzilishi wa shirika la Babymoon linalosaidia watoto njiti.

"Nilimueleza kuwa Afrika kuna tatizo kubwa la vifo vya watoto hawa, nikamshawishi aje Afrika na Tanzania kufanya mradi huu," anasema Dk. Deborah.

Pia, katika hospitali za Uholanzi zimesheheni vifaa vyote muhimu vya kuhudumia mfumo wa kangaroo, ambayo Dk. Maufi anashauri mtindo huo kutumika katika nchi zinazoendelea ikiwamo kubeba watoto kwa kutumia khanga na vitenge.

Anashauri :"Elimu itolewe kwa mama yeyote mjamzito hapa Tanzania, itasaidia kupunguza vifo watoto wachanga. Kama unavyojua hakuna anayejua mjamzito atajifungua mtoto miezi ikikamlika au la."



Mama wa njiti aliyeko katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

> **Watoto hawa wanaozaliwa kabla ya wakati hukumbwa na matatizo katika ukuaji, wengine hupata ulemavu, wana mzio, wanahitaji uangalizi maalum.**

Balozi huyo wa watoto wachanga anasema, aliamua kujikita katika eneo la watoto kwa miaka miwili alipogundua matatizo yanayowakumba njiti.

**MDAU MKUU**

Mkurugenzi Mkuu wa taasisi ya Doris Mollel Foundation (DMF), inayojishughulisha na kusaidia watoto njiti, Doris Mollel, anadokeza kuwa vifo vya njiti ndio imechagia kuanzishwa asasi hiyo anayoiendesha na kutoa elimu kwa jamii.

"Mimi nilizaliwa nikiwa na gramu 900 miaka 29 iliyopita. Mimi Kulwa nina pacha mwenzangu. Nimefanya kazi hii kwa miaka mitano sasa, nashirikiana na wadau kufikisha elimu kuhusu watoto hawa na itaweza kupunguza vifo vyao.

"Watoto hawa wanaozaliwa kabla ya wakati hukumbwa na matatizo katika ukuaji, wengine hupata ulemavu, wana mzio, wanahitaji uangalizi maalum," anasema Doris.

Anasema kaulimbiu ya mwaka katika siku ya watoto njiti duniani inayofanyika Novemba 17, kila mwaka asasi hiyo imeadhimisha kwa kushirikiana na wadau na Wizara ya Afya, kuhimiza makuzi na malezi bora ya watoto hao. Doris anasema, kaulimbiu ni 'pamoja kwa ajili ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati kujali kesho yao'.

Anafafanunua kuwa maadhimisho hayo yamelenga kukumbuka watoto ambao kati ya wachanga milioni 15 wanaozaliwa duniani, milioni moja wanapoteza maisha duniani.

Mama huyo anaeleza kuwa katika uzoefu wake na hata akabuni haja ya kusaidia watoto njiti katika kupata huduma muhimu za afya.

**BIMA AFYA?**

Huku akitoa wito kwa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Doris anautaka mfuko uwatambue watoto hao kwa kuwa na kifurushi maalum cha matibabu yao.

Anasema, hakuna bima ya afya inayotolewa kwa kundi hilo, licha ya kuwapo hitaji kitabibu watoto hao kutakiwa kukaa hospitalini kwa zaidi ya miezi mitatu na mama zao, ili waongezeke uzito na kupatiwa dawa maalum.

"Kumlea mtoto njiti ni gharama kubwa, mashine kuwasaidia kupumua hutumia umeme, kuna njiti wanaozaliwa chini ya kilo moja, mashine ya oksijeni moja ya hospitalini ni Sh. milioni 3.5," anasema.

Rai yake ni kuelekeza ombi la bima, isaidie kubeba gharama za mtoto njiti, kwani mama huchangia mfuko huo akiwa na matarajio atajifungua kama kawaida na inapotokea anajifungua njiti anahitajika kutoa pesa.

"Mfano, maziwa Sh. 500,000 hadi 700,000, mashine za joto ni shilingi milioni 3.5, watoto hawa huduma zao ni za mamilioni. Ili kuwa na chumba maalum cha kulea watoto njiti, kinahitaji si chini ya Sh.milioni 60," anasema Doris.

Pia, anagusia mahitaji ya vifaa maalum vya kuwasaidia kupumua, kama dawa za kukomaza mapafu zenye gharama kubwa.

"Watoto hawa 'immunity' (kinga) yao inakuwa iko chini, sababu siku hazikutimia kukumbwa na maradhi hata baridi ni tatizo kwao.

"Kwa mtoto njiti, kile ambacho kawaida kwa aliyezaliwa siku zimetimia kwao ni shida, huhitaji maziwa maalum kuwasaidia kuongezeka kilo na mipira ya kupumulia," anaeleza.

Katibu Mkuu, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Prof. Mabula Mchembe kwenye maadhimisho yanayowahusu njiti, anasema vifo vya watoto wachanga wakiwamo njiti ni tatizo kubwa nchini na vinachangia asilimia 40 ya vifo vyote vya watoto walio katika umri chini ya miaka mitano.

**HALI YA VIFO**

Katika hotuba ya katibu mkuu iliyosomwa na Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Prof. Andrea Pembe tarehe 17, mwezi uliopita, anasema takwimu za mwaka 2015 na 2016 zinaonyesha kati ya watoto 1,000 wanaozaliwa hai, 25 wanapoteza maisha kabla ya kutimiza siku 28.

"Vifo hivyo, vinachangia takribani asilimia 40 ya vifo vyote vya watoto chini ya miaka mitano kwa takwimu za TDHS (demografia ya afya) mwaka 2015 na 2016, vinavyotokea nchini," anasema.

Prof. Pembe ananukuu taarifa za Wizara ya Afya, imwaka 2018 kulikuwapo vifo vya watoto wachanga 11,524 vilivyotolewa taarifa na mwaka jana 9,681.

Anasema takwimu zinaonyesha vifo vya watoto wachanga, vinaangukia kwa wenye matatizo yanayoambatana na kuzaliwa wakiwa na uzito pungufu kabla ya wakati.

"Mtoto kuzaliwa kabla ya wakati 'premature' ni kabla ya mimba kukamilisha wiki 37 za ujauzito. Hapa nchini tatizo hili ni kubwa, Taarifa ya 'World Population Prospects' ya mwaka 2013 inaonyesha Tanzania ni kati ya nchi 20 duniani zinazoongoza kwa kuzaliwa watoto njiti wanaofikia watoto 213,500 kwa mwaka," anasema Prof. Pembe.

Ana ufafanuzi kuwa, watoto milioni 15 wanazaliwa njiti kila mwaka duniani wakiwa katika hatari ya vifo, kwa sababu ya kushindwa kutunza joto mwilini, wanapumua kwa tabu, kupata maambukizi ya bakteria na kuwa na viungo dhaifu.

"Tutie nguvu kuchagiza Halmashauri zote na wadau katika kuongeza vyumba vya matibabu ya watoto wachanga wagonjwa (Neonatal Care Unit), kujenga uwezo wa watoa huduma kwa ajili ya huduma bora za watoto wachanga wakiwamo watoto njiti," anahitimisha.

AFYA

# Shinyanga inavyochechemea ndani ya tope la utapiamlo sugu kimkoa

## • Kila kundi 190, watoto 22 wanasa • Tingatinga World Vision lawanasua

**Na Shaban Njia,** KISHAPU

WASTANI miaka mitano iliyopita, shida ya utapiamalo ambayo kimsingi ni uhalisia kimwili na athari ya kuiweka dhaifu Mkoa Shinyanga, ulikuwa juu kupindukia miaka kwa wastani wa asilimia 59,

Sababu kuu ni lishe isiyo bora au vyakula visivyokuwa na virutubisho na wajawazito kushindwa kula vyakula vinavyoongeza damu mwilini.

Leo hii walau kuna lugha tofauti, hali imepungua hadi asilimia 30.2, ingawa si nafuu ya kiasi kikubwa. Ni baada kutekelezwa mradi wa kukabili utapiamlo.

Pia, hadi mwaka juzi mkoa uliandamwa na udumavu kwa watu wake na kukonda kiwango cha asilimia nne, hali inayochangia kiafya mtoto kuwa na kimo kifupi.

Mikoa mingine yenye hali mbaya ya utapiamlo kitaifa kwa mujibu wa takwimu zilizopo ni Njombe (53.6%), Rukwa (47.9%), Iringa (47.1%), Songwe (43.3%), Kigoma (42.3%) na Ruvuma (41%).

Sababu ya kuongezeka ugonjwa huo zinatajwa kuwa ukosefu wa lishe bora au kula vyakula visivyokuwa na virutubisho na wanawake wajawazito kutokula viini lishe sahihi na vinavyoongeza damu mwilini.

### KILICHOKO SHINYANGA

Shirika lisilo la kiserikali la World Vision Tanzania, hivi sasa wanatekeleza mradi wa uboreshaji huduma za lishe katika kuimarisha afya ya mama na mtoto(ENRICH) kwa ufadhili wa serikali ya Canada, katika mikoa ya Shinyanga na Singida.

Kinachofanyika sasa, ni kuwafundisha wanaoibanika kuwa na watoto wenye utapiamlo, namna ya kuandaa chakula chenye lishe.

Mradi huo uliopo katika halmashauri za Ikungi na Manyoni (Singida) na Halmashauri za Kahama Mjini, Shinyanga Vijijini na Kishapu (Shinyanga), unalenga kupunguza vifo vya wajawazito na watoto chini ya miaka mitano na unatarajia kukamilika mwaka ujao.

### WARATIBU MIPANGO

Denis Madeleke, Mratibu wa Lishe Mkoa Shinyanga, anasema kukosa elimu ya uandaaji chakula chenye lishe kijijini Wishiteleja Kata ya Mondo, Kishapu, kumesababisha wagonjwa wa utapiamlo na wajawazito wenye upungufu wa damu.

Pia, anasema mila na desturi kwa baadhi ya jamii zimekuwa zikiwaandamiza wajawazito kukosa vyakula vyenye lishe sahihi jamii ya wanyama na katika ukuaji mtoto tumboni, hali inayomjengea kasoro katika



Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Mondo, Halmashauri ya Kishapu, Dk. Christian Ngowi akimpima uzito mtoto. **PICHA: SHABAN NJIA**

> **Nakula makapi ambayo hayana virutubishi na ndio sababu ya kuwapatia elimu ya namna ya kulima na kuandaa vyakula bora.**

ukuaji mtoto.

Anasema, kijiji cha Wishiteleja kina watoto 190 wenye umri kuanzia miezi sita hadi miaka miwili, kati ya 71 walifanyiwa tathmini na kubainika 22 wana utapiamlo, baada ya kukosa lishe bora

Madeleke anakumbusha ukuaji mtoto unaanza wakati mimba inapotunga hadi siku zake 1000, kuwapo utapiamlo na udumavu katika siku hizo ni kukaribisha tatizo la afya la kudumu kwa mtoto.

Dk. Frank Mtimbwa, Mratibu wa Mradi wa ENRICH kutoka asasi ya World Vision Tanzania, anasema utanufaisha zaidi ya wananchi 1,697,785 wa mikoa hiyo tajwa na ikiwa na wadau 1, 105, 606, sawa na asilimia 65 kutoka Shinyanga.

Anafanya mnyambuo wa wanawake 248,104 na wanaume 130,448; wasichana 103,173 na wavulana 107,383 na makundi maalumu wakiwa 516,497.

### MGANGA MFAWIDHI

Maganga Mfawidhi wa Zahanati ya Mondo, Christian Ngowi, anasema kipindupindu na kuhara katika kijiji cha Wishiteleja, kimepungua kwa asilimia mbili, baada ya wananchi kupewa elimu ya umuhimu wa kunawa mikono.

Anasema, kabla hajapata elimu ya kunawa mikono, magonjwa yaliyoripotiwa katika zahanati yalikuwa ya mlipuko na hasa kipindupindu na kuhara kwa watoto chini ya miaka mitano.

Ngowi anasema, ugonjwa huo ulifika mpaka asilimia 18 sawa na wadogo chini ya miaka mitano wanaozidi 216 na baada ya kutolewa elimu ya umuhimu wa kunawa pekee, ghafla ugonjwa ulishuka hadi asilimia mbili.

"Kata hii ina watoto zaidi ya 1,190 chini ya miaka mitano. Wengi waliokuwa wakiripotiwa zahanati walikuwa wakiumwa ugonjwa wa kipindipindu na kuhara na hii ni kwa sababu ya mazingira machafu nyumbani, hasa mama kumshika mtoto na kumnyonyesha kabla ya kunawa mikono au baada ya kutoka maliwato, " ansema Ngowi.

### OFISA KILIMO

Ofisa Kilimo wa Kata ya Mondo, Pius Maganga, anasema wameanzisha bustani za mboga kwenye kaya 22 zilizobainika kuwa na utapiamlo, lengo ni kupambana na ugonjwa huo utokanao na ulaji vyakula visivyokuwa na lishe.

Anasema, kinachofanyika sasa ni kuwafundisha kulima vyakula vinavyopatikana katika maeneo yao, hasa kutengeneza bustani za ukubwa wa mita tatu, wanazoweza kuzihudumia.

Pia, anataja ukame ni tatizo kwa kukamilika mradi wa kufanya kata nzima kuwa na bustani za mboga. Maganga anafafanua: "Wanatumia aina ya mkalanga, wanaichuma na kuiweka juani inakauka kwanza na kabla ya kuipika na kupoteza vitamini A.

"Nakula makapi ambayo hayana virutubishi na ndio sababu ya kuwapatia elimu ya namna ya kulima na kuandaa vyakula bora."

### WANUFAIKA VIAZI LISHE

Magdalena John, mwanawake aliyebainika kuwa na mtoto mwenye utapiamlo, anasema mwanawe alikuwa na uzito chini ya kilo saba na baada ya kupewa elimu ya uandaaji chakula sahihi na kulima bustani za mboga, uzani uliongezeka kufikia kilo 10.

Anasema, alipata mafunzo ya kuandaa chakula chenye virutubishi kwa kutumia vinavyopatikana kirahisi ndani ya kata yao, inayomsaidia mtoto wake kuendelea kuimarika kiafya na kuongezeka kimo, akilinganishwa na awali.

Dogani Mwanzalima, mkulima wa viazi lishe katika Kijiji cha Negezi Kata ya Ukenyenge, ana ombi kwa serikali iwatafutie masoko ya viazi lishe nje, ili kuongeza kasi ya uzalishaji na kupunguza utapiamlo.

Anasema, katika msimu uliopita mwaka jana, walilima jumla ya matuta 25 ya viazilishe na wakavuna tani nne, walitafutiwa masoko na World Vision Tanzania katika kiwanda cha kuongeza thamani Maswa.

Mwanzalima anaendelea:"Nilipata Sh. milioni 1.76 na kukubaliana na wake zangu, tukanunua ng'ombe wawili wa kilimo, kila mmoja Sh. 500,000 na ngombe mmoja wa maziwa, kwa Sh. 380,000 kwa ajili ya maziwa ya watoto, ili kuendelea kuimarisha afya zao."

Mkulima Veronica Amos, anasema wamekuwa wakizalisha viazilishe na kuuza kwa bei ya Sh. 6,500, kwa kila kilo katika Kiwanda cha Kuongeza Thamani ya Viazilishe Maswa.

*•Soma makala zaidi uk. 14.*

AFYA

## OFISA LISHE PWANI:

# Tunapigana vikumbo kujichomoa utapiamlo

• Kibaha walia shida imejificha shuleni

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SALAMA ya mtoto mchanga na lishe yake sahihi iko wapi kumnusuru kiafya? Ofisa Lishe Mkoa wa Pwani, Pamela Meena, anataja siku 1,000 za kupambana na udumavu kwa watoto.

Hisabati sahihi ni safari yote ujauzito wa mama, hadi mtoto mzaliwa anapofika umri miaka miwili. Hapo kunatajwa hatari ya mama kuzaa mwenye udumavu, pale anapokosa elimu ya kutosha ya malezi. Usahihi unahimizwa na Ofisa Lishe ni namna vyakula anavyotakiwa kula akiwa mjamzito na katika kipindi cha kunyonyesha.

Pamela anafafanua mama asipomnyonyesha vizuri mwanawe kwa kipindi cha miezi sita ya awali na kumpa vyakula vya nyongeza kwenye makundi matano, mtoto anaangukia udumavu wa mwili.

Anarejea takwimu za kimkoa kwamba una wakazi 1,295,267 na kati yao watoto wako 194,433. Katika kundi hilo anasema, hali ya udumavu umefikia asilimia 23.8 na kitaifa wako asilimia 31.8 ambayo ni watoto milioni tatu. Pamela anasema, Mkoa wa Pwani una vituo vya huduma za afya 337 na vyenye huduma ya mama na mtoto viko 288, watoto wenye uzito pungufu wanaelezwa kufikia asilimia 8.9 na wenye ukondefu asilimia nne.

### LISHE DUNI

"Udumavu huathiri ukuaji wa mwili na akili na hali hii inaweza kurekebishwa ndani ya siku 1000 za makuzi ya mtoto, kuanzia kutungwa mimba hadi anapofikia umri miaka miwili," anaeleza Ofisa Lishe.

Pamela anatoa angalizo kuwa wanawake wajawazito, pale watakaposisitizwa kuhudhuria kliniki mapema, wanapojitambua au wanapofanya uamuzi ya kubeba mimba. Anasema, kitendo cha kuhudhuria kwenye vituo vya afya kitawawezesha kupata elimu ya mlo salama utakaomuwezesha mtoto kukua vizuri na mama mjamzito kuwa na afya nzuri.

"Jamii kubwa ya Watanzania tumeacha ulaji wetu wa kitamaduni na kupenda ulaji wa mataifa ya kigeni, hali inayosababisha kula aina moja au mbili, ambao madhara yake yanaonekana kwa watoto chini ya miaka mitano na wajawazito," anasema.

### WALE NINI?

Ofisa Lishe huyo anaeleza vyakula vinavyotakiwa kulia, ni katika makundi matano ambayo ni vyakula vya nafaka kama mahindi, mtama, mchele, ulezi, ngano, uwele na shairi, zikioanishwa na ndizi mbichi na zile za mizizi (viazi, mihogo na magimbi) ambavyo vyote vinaongeza nguvu mwilini.

Kundi la pili la vyakula asili ya nyama na jamii ya kunde, ambavyo ni pamoja na jamii ya viumbe wadogo, kama vile senene na kumbikumbi, ndege (kuku, bata, kware, kanga).

Aidha, Pamela anataja nyama za mbuzi, ng'ombe, kondoo, samaki na mazao mengine yatokayo baharini, vyote vikilenga ujenzi wa mwili.

Kundi la tatu ni vinavyokinga mwili, jamii za mboga, karoti, nyanya chungu, mlenda na mboga zote za majani, huku kundi la nne linajumuisha matunda yote ya porini, yanayolimwa au kupandwa shambani.

Analitaja kundi la tano linaangukia vyakula vya mafuta na sukari, ambavyo nafasi yake mwilini ni kutia nguvu.



Mkuu wa Wilaya ya Rufiji, Patrick Sawala, katika hafla inayohusu lishe.

> **Wanafunzi wanatofautiana hali zao kimaisha wapo wanaoishi na mzazi mmoja hata kupata Sh. mia anapoenda shuleni ni mtihani kwao, pia nyumbani anakotoka hajapata hata chai.**

### ANAVYOJIHAMI MJAMZITO

Ofisa lishe Pamela, anasisitiza mjamzito ahakikishe anapata mlo kamili wenye vyakula mchanganyiko na angalau apate milo mitatu kwa siku.

Mama anatakiwa kuongeza idadi ya milo, kutoka mitatu hadi mitano na anatakiwa kula usiku anaponyonyesha, ili mtoto aweze kupata maziwa ya kutosha yatakayomwezesha mtoto kunyonyesha mara nane au zaidi kwa siku.

"Mtoto akifikisha miezi sita apewe vya kila vya ziada, pia akishaanza kula, isiwe sababu ya kuachishwa kunyonya, kwani anatakiwa kunyonya hadi miezi 24.

"Udumavu unakuja endapo kipindi cha miaka miwili tangu mimba kutungwa, mama asipofuata mtiririko wa ulaji na ulishaji wa mtoto, ikumbukwe kuwa udumavu huathiri ubongo na ukuaji wa mwili wa mtoto," anasisitiza Pamela.

Aidha, Ofisa Lishe huyo anasema mtoto mwenye udumavu hawezi kusoma vizuri, pia anakosa uwezo wa kupambanua, ikiwamo darasani.

Pamela anataja majibu ya kukabili kasoro hiyo kabla ya umri miaka miwili, akijumuisha mahudhirio ya kliniki zitakazomuwezesha mama kupata elimu ya unyonyeshaji na lishe kwa mtoto.

### UTAPIAMLO SHULENI

"Watoto wanaoanza shule kuanzia darasa la awali, wana uwezo wa kupata utapiamlo kama hatapata chakula na kushinda na njaa kwa muda mrefu, hawezi pia kukua vizuri kimaumbile," anasema.

Katika hilo, Ofisa Lishe huyo anasisitiza watoto kupewa mlo kamili shuleni kwa kushirikiana na wazazi, kunaimarisha stadi zao.

Ili kufanikisha hilo, anasema wanafunzi kuanzia darasa la nne hadi la sita wanafundishwa upandaji mboga na matunda, kunakoweza kulimwa shuleni na watoto inawasaidia majumbani katika ukuaji wao.

### DC KIBAHA

Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Martine Ntemo, anaeleza hali ya udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano wilayani kwake imepungua kutoka asilimia 12.5 mwaka 2015/2016 hadi asilimia 4.5 katika mwaka 2019/2020.

Pia, anaueleza utapiamlo kwa watoto chini ya miaka mitano umepungua kutoka asilimia 18.7 mwaka 2015/2016 hadi asilimia 16 mwaka 2019/2020.

Sambamba na hilo, kuna suala la uzito pungufu kwa watoto chini ya miaka mitano, kwamba limepungua kutoka asilimia 7.9 mwaka 2015/2016 hadi asilimia 6.3 mwaka 2019/2020.

### WENYEJI WA MTAA

Mkazi wa Mailimoja, Kibaha Philemon Mabuga, anasema suala la kuwa na chakula shuleni ni la kuliwekea mkakati kwani ni muhimu kwa wanafunzi wawapo shuleni.

"Wanafunzi wanatofautiana hali zao kimaisha wapo wanaoishi na mzazi mmoja hata kupata Sh. mia anapoenda shuleni ni mtihani kwao, pia nyumbani anakotoka hajapata hata chai.

"Anapofika shule hakuna chakula mpaka mchana, lazima adumae hawezi kufikiria masomo, hawezi kufaulu kwa kuwa akili haiwezi kufikiri kitu akiwa na njaa," anasema Mabuga.

Rai yake ni wazazi kushirikishwa na uongozi wa serikali za mitaa, kwa kuitishwa mikutano na suala la chakula shuleni likawe ajenda inayotiliwa mkazo. Mabuga anashauri kuwapo sheria kwenye halmashauri nchini, ili kufanikisha kuwapo chakula shuleni, jambo litakalowaondolea mzigo walimu na uongozi wa shule.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Tangini, katika Halmashauri ya Mji Kibaha, Primin Gama, anasema suala la chakula shuleni linapaswa kuanza na wanaokuwa na muda mrefu masomoni, mathalan walioko darasa la sana.

"Miaka ya sabini (1970) tulipokuwa tunasoma, tulikua tunakula shuleni kutokana na baadhi yetu kuishi mbali na shule ikianza tena itasaidia, kwani wapo watoto wanatoka asubuhi hawajapata hata chai nyumbani kwao na hivyo kuwa makini darasani kwao ni kikwazo cha ufaulu," anasema.

Mwenyekiti huyo anaahidi ajenda ya chakula shuleni inatarajiwa kujadiliwa katika vikao vya mitaa vitakavyowezesha uhamasishaji, unaombatana na elimu yake, ili kuwezesha kupita kirahisi katika vikao vya halmashauri, Kibaha.





Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, akiongoza kikao cha utendaji kazi cha maofisa wakuu wa makao makuu ya jeshi hilo, jijini Dodoma jana, kilichojadili na kufanya tathmini ya mafanikio, changamoto kwa kipindi kilichopita na kuweka mikakati ya kutekeleza kazi za polisi kwa ufanisi zaidi katika kulinda usalama wa raia na mali zao. Wengine ni makamishna wa jeshi hilo. **PICHA: JESHI LA POLISI**

# RC azipa taasisi mwezi kuandaa mpango wa uwekezaji na makazi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ametoa mwezi mmoja kwa taasisi zinazotoa huduma za kijamii mkoani humo, kuandaa mpango maalumu wa kupeleka huduma kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji na makazi ili kuhamasisha wawekezaji.

Taasisi hizo ni Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), Shirika la Umeme (TANESCO) na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma (DUWASA). Akizungumza jana kwenye ziara ya kukagua maeneo yote yaliyoiva kiuwekezaji na makazi ya Nala, Nala IFM, Mahungu, Michese, Mkalama na Iyumbu jijini hapa, Dk. Mahenge alisema wawekezaji wengi hawajitokezi kwa sababu hakuna huduma za kijamii katika maeneo hayo.

"Wawekezaji wanasita kuja kuwekeza katika maeneo haya, huduma za kijamii hamna wanahofia kukwama kwa shughuli zao, pia kama unavyoona kuna watu wamejenga majumba mazuri, lakini hawana huduma muhimu huku ni kukatishana tamaa," alisema.

Aliagiza ndani ya siku 30 kila taasisi ihakikishe inaandaa mpango mahususi na kupeleka ofisini kwake namna zilivyojiandaa kupeleka huduma za kijamii katika maeneo ya uwekezaji na makazi ya wananchi.

"Nataka kila taasisi ije kwangu na mpango imejipangaje kupeleka huduma katika maeneo hayo, kama ni TARURA uje na mpango umejipangaje kuhakikisha barabara zinapitika wakati wote, kama ni DUWASA umejipangaje maji yapatikane ili tusiwacheleweshe wawekezaji wetu," alisema.

Alizitaka taasisi hizo kuhakikisha zinafanya kazi kwa kushirikiana ili kufikisha huduma bora kwa wananchi kwa wakati.

"Pia hakikisheni hamtakuwa kikwazo kwa wawekezaji na wananchi kukosa huduma hizo za kijamii," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Joseph Mafuru, alisema eneo la uwekezaji la Nala lina ekari 2,713 na wameshalipa fidia kwa wananchi ya Sh. bilioni 3.5, na eneo linaviwanja 189 kwa ajili ya viwanda na vina ukubwa unaoanzia ekari moja hadi ekari 250.

Alisema eneo hilo ni zuri kwa wawekezaji kwa sababu limeunganishwa na barabara za mzunguko (ring road) zitakazolizunguka Jiji hilo na tayari wameshaanza kupokea maombi kutoka kampuni mbalimbali zikiwamo za TBL, Serengeti Brewers na wafanyabiashara kutoka mikoa ya Mwanza, Arusha na Dar es Saalam.

Aidha, alisema kuwa kwa maeneo ya makazi tayari wameshapima na wapo katika hatua mbalimbali za umilikishwaji na kutoa vibali vya ujenzi katika maeneo ya Mahungu, Michese, Iyumbu na eneo linalokuwa kwa kasi la Mkalama jirani na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

# CKHT yajizatiti kufundisha kwa viwango

**Na Vincent Mpepo,** OUT

CHUO Kikuu Huria cha Tanzania (CKHT) kimejizatiti kufundisha kwa viwango vya kitaifa na kimataifa ili wanufaika watimize mahitaji yao ya kielimu na kukidhi kwenye soko la ajira.

Mkurugenzi wa Huduma za Maktaba wa Chuo hicho, Dk. Athumani Samzugi, aliyasema hayo katika mafunzo elekezi ya siku tatu kwa wanafunzi wapya na wanaoendelea ambayo yalifanyika kwenye vituo vyote vya mikoa vilivyopo nchini.

Alieleza kuwa chuo hicho kimedhamiria kutoa huduma zote muhimu ikiwamo ya kimaktaba kama sehemu ya kufanikisha malengo ya wahitaji ili kurahisisha usomaji wao.

"Tuna maktaba ya kianalojia na kidijitali ambazo ukizitumia vizuri zitakusaidia katika usomaji na ujifunzaji, hivyo kufanya maisha ya kitaaluma hapa chuoni kuwa mepesi," alisema.

Alisema maktaba ndio moyo wa taasisi yoyote ya kitaaluma hivyo waitumie vizuri na kwamba mihadhara haiwezi kuwapatia maarifa yote muhimu bila kuongezea kutoka maktaba ili kupanua wigo wa uelewa kwa mada husika.

Naye, Mratibu wa Ufundishaji na Kujifunza wa chuo hicho, Dk. Lawi Yohana, aliwataka wanafunzi hao kutambua dhana za elimu huria na masafa ambazo zinakitofautisha chuo hicho na vyuo vingine nchini na vingi katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

"Elimu huria na masafa inajitanabaisha kwa kutoa fursa zaidi kwa mwanafunzi kupata elimu bila vikwazo kwa kutambua maarifa alinayo mwanafunzi na haitegemei mkufunzi au mhadhiri kama nyenzo kuu ya mchakato wa usomaji, ujifunzaji na badala yake inajikita kwa mwanafunzi mwenyewe," alisema. Alisema elimu ya chuo hicho inamsaidia mwanafunzi kupata umahiri katika ngazi mbalimbali utakaomsaidia kumudu vyema utatuzi wa vikwazo kwenye mazingira yake ya kazi.

Kwa upande wake, kiongozi wa serikali ya wanafunzi wa chuo hicho katika kituo cha Mkoa wa Dodoma, Ismail Mussa, aliwahimiza wanafunzi hao umuhimu wa kuwajibika kwa kufuata taratibu na sheria za chuo, ili kuepuka kwenda kinyume cha taratibu zitakazowakwamisha kufikia malengo yao.

"Ukikamatwa kwenye mtihani na kitu kisichotakiwa na ukaniarifu nitakupa sababu za kisiasa, lakini mwisho wa siku maamuzi ya chuo yatafuatwa kwa wewe kutekeleza adhabu utakayopangiwa," alisema.

Alisema bado wanafunzi wanapaswa kuishi kwa kufuata sheria na taratibu za chuo kwa kusoma kwa bidii ili kujiepusha kutaathiri maendeleo yao kitaaluma.

# Hospitali ya Mkapa yajipanga matibabu moyo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

HOSPITALI ya Benjamin Mkapa imejipanga kuhakikisha huduma za matibabu ya moyo ikiwamo kuweka betri kwenye moyo wenye mapigo ya chini zinatolewa kwa ufanisi.

Hatua hiyo ilielezwa jana na Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Moyo, Dk. Peter Kisenge, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari juu ya matibabu ya uzibuaji mirija ya moyo iliyoziba.

Alisema hospitali hiyo ina mtambo wa kisasa ambao umegharimu zaidi ya Sh. bilioni nne na unasaidia pia kuweka betri za moyo kwa mgonjwa ambaye mapigo yake yapo chini 50 kwa dakika.

Alibainisha kuwa hospitali hiyo ina madaktari wazuri waliobobea na wanafanya matibabu hayo.

"Matibabu ya moyo ni gharama kubwa sana kama mgonjwa angepelekwa kutibiwa nje kwa kutumia kizibua njia angegharimu Sh. milioni 20, na tukimfanyia hapa kwetu ni Sh. milioni sita," alisema.

Alieleza kuwa nchi ilikuwa inapoteza zaidi ya Sh. bilioni 30 kwa ajili ya matibabu ya magonjwa mbalimbali ambayo walikuwa wakipelekwa nje.

"Tunadhamira ya kwenda mbali zaidi kuhakikisha sasa tunaanza kutoa huduma ya kuhamisha moyo kutoka upande ulipo na kuweka mwingine, na hayo ndio malengo yetu kwa sasa," alisema.

Alitoa wito kwa Watanzania kutumia huduma za hospitali hiyo ambayo ina wataalamu waliobobea ikiwamo ya uzibuaji mirija kwenye moyo iliyoziba.

"Tunaomba wananchi wenye matatizo kama haya waonane na madaktari kwenye mikoa yao wawafanyie uchunguzi na kuhamishia kwenye hospitali hiyo kwa ajili ya matibabu," alisema.

Alisema mtambo huo kwa jana tangu uanze kufanya kazi umehudumia wagonjwa 18.

"Ugonjwa wa moyo kwa sasa ndio wa kwanza unaochangia vifo vingi kwa wagonjwa wanaolazwa, ambapo kati ya watu 10 wanaolazwa hapa hospitali sita wana matatizo ya moyo," alisema.

Naye Mkazi wa Ngara mkoani Kagera, James Tabindi, ambaye ni miongoni mwa wagonjwa waliopata huduma, aliishukuru serikali kwa uwekezaji wa mitambo hiyo ambayo imesaidia kupunguza idadi ya Watanzania kutibiwa nje ya nchi.

"Wengine walikuwa wanaenda India, wengine Muhimbili ambapo unakutana na foleni kubwa, lakini uwapo wa hospitali hii imesaidia unakuja siku mbili unatibiwa na kurudi nyumbani," alisema.



## Polisi yataja mafanikio kukabiliana ukatili kijinsia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limeeleza mafanikio yake katika kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo ubakaji na ulawiti wa watoto katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari mpaka Novemba mwaka huu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, aliwaambia waandishi wa habari juzi kuwa mwaka huu jeshi hilo limewakamata na kuwafikisha mahakamani watu kadhaa waliobainika kufanya vitendo hivyo vya ukatili.

Alisema kuanzia mwezi Januari mpaka sasa kesi tatu za ubakaji na ulawiti zimeshatolewa hukumu mahakamani na wahusika wamehukumiwa vifungo mbalimbali kwa mujibu wa sheria za nchi.

Alisema kijana wa kwanza aliyekumbana na adhabu hizo ni James Pondo (27), mkazi wa Wilaya ya Chunya ambaye alikamatwa Februari 5, mwaka huu kwa tuhuma za kumlawiti mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka 10.

Alisema kijana huyo amehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela baada kuthibitika kuwa alifanya kitendo hicho dhidi ya mtoto.

Alisema kijana mwingine aliyekumbana na adhabu hiyo ni Said Mrisho (21), mkazi wa Wilaya ya Chunya aliyekamatwa Machi 20, mwaka huu katika Kijiji cha Mazimbo akituhumiwa kumlawiti mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka saba.

Alisema kijana huyo alifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Chunya na kuhumumiwa kifungo cha maisha jela baada ya ushahidi kuonyesha kuwa alifanya unyama huo. Kamanda Matei alimtaja Fadhil Mwambapa (28), mkazi pia wa Wilaya ya Chunya ambaye alikamatwa na jeshi hilo Aprili 18, baada ya kutuhumiwa kumbaka mtoto wa kike mwenye umri wa miaka 13.

Alisema kijana huyo alihukumiwa kwenda jela miaka 30 baada ya mahakama hiyo kuthibitisha kuwa alifanya unyama huo.

"Sasa hivi tumeweka polisi katika kila kata, hivyo niwaombe wananchi waendelee kushirikiana na maaskari hawa katika kutokomeza uhalifu ikiwamo ukatili dhidi ya wanawake na watoto, nimeamua kuyasema haya kwa sababu tupo ndani ya muda wa siku 16 za kupinga ukatili," alisema Kamanda Matei.

Vilevile, aliwataka wananchi kuendelea kutoa taarifa kwenye vyombo mbalimbali wanapobaini vikundi ambavyo vinavyofanya shughuli zisizoeleweka vidhibitiwe mapema.

Aliwataka wazazi na walezi kuhakikisha wanawalinda watoto wao dhidi ya vibaka pamoja na kuwalea katika maadili mema, ili wakikua wasijiingize kwenye vitendo viovu na kuwa kero kwa jamii.

# Mzumbe kumuaga rasmi Jaji Samatta

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JUMUIYA ya Chuo Kikuu Mzumbe, imeanza rasmi kumuaga Mkuu wa Chuo hicho, Jaji mstaafu Barnabas Samatta ambaye anamaliza muda wake na kumkaribisha Rais mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Ally Mohamed Shein, ambaye aliteuliwa hivi karibuni kuongoza chuo hicho.

Akizungumza wakati wa mahafari ya 19 ya chuo hicho katika Ndaki ya Mbeya, Mwenyekiti wa Bodi, Prof. Mathew Luhanga, alisema Jaji mstaafu Samatta, amekiongoza chuo hicho kwa mafanikio makubwa katika kipindi cha miaka 12.

Alisema jumuiya ya chuo hicho itaendelea kuyaenzi mazuri ya kiongozi huyo na kwamba jumuiya hiyo ina imani kubwa na mkuu mpya wa chuo, Dk. Shein, kutokana na kuiongoza Zanzibar kwa mafanikio.

"Mkuu wetu umekiongoza chuo hiki kwa muda mrefu na kwa mafanikio makubwa sana, maendeleo ambayo chuo kinayo kwa sasa ni kutokana na uwapo wako, hivyo tunampongeza Rais Magufuli kwa kukuamini na sasa amemwamini Dk. Shein ili akupokee kijiti hiki cha kuiongoza taasisi yetu," alisema Prof. Luhanga.

Alisema kwa mujibu wa utaratibu, Jaji Samatta, atamaliza rasmi muda wa kukiongoza chuo hicho mwezi Januari mwakani na ndio utakuwa muda mwafaka wa Dk. Shein kukabidhiwa kijiti hicho.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Lugano Kusiluka, alisema asilimia 60 ya umri wa Chuo Kikuu Mzumbe imeongozwa na Jaji Samatta kama Mkuu wa Chuo na kumpongeza kwa kasi kubwa aliyoifanya.

Alisema chuo hicho kilipanda hadhi na kuwa Chuo Kikuu mwaka 2001 na Jaji Samatta, aliteuliwa mwaka 2009 kukiongoza kuwa Mkuu wa Chuo na kufikia mwezi Januari atakuwa ametimiza miaka 12 ya kukiongoza.

Alisema Jumuiya ya Chuo hicho inamtakia maisha na majukumu mema kwingineko atakakokwenda kulitumikia taifa na wataendeleza mazuri yote aliyoyaanzisha ili kufikia malengo ya kuzalisha wasomi wengi.

Prof. Kusiluka alisema wakati chuo hicho kinaanza kilikuwa na wanafunzi 405 pekee na programu zilikuwa mbili, mpaka sasa wanafunzi wameongezeka na idadi ya programu imeongezeka.

"Mwaka huu pekee tumesajili wanafunzi 11,967, lakini programu zinazofundishwa zimefika 12 na tutaendelea kuongeza kadri tutakavyoyaona mahitaji ya taifa letu, hivyo haya mafanikio tuliyoyafikia, Jaji Samatta ana mchango mkubwa sana," alisema Prof. Kusiluka.

Katika hatua nyingine Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo hicho, Prof. Luhanga, alimpongeza Rais Magufuli kwa kuonyesha ujasiri mkubwa wakati wa mapambano dhidi ya virusi hatari vya corona vinavyosababisha homa kali mapafu (Covid-19).

Alisema mpaka sasa mataifa mengine yanaendelea kufunga baadhi ya shughuli za kijamii kutokana na virusi hivyo kuendelea kuyasumbua, lakini Tanzania shughuli zinaendelea zikiwamo zinazokusanya watu wengi.



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, SACP Ulrich Matei (kushoto), akiangalia baadhi ya vitu vya wizi vilivyokamatwa na jeshi hilo, katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya, wakati wa msako maalumu uliofanyika wiki iliyopita. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wenye VVU watakiwa kutaja wapenzi wao wapewe dawa

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MKOA wa Mbeya umeanzisha mpango maalumu wa kuwataka watu wote wanaopimwa na kubainika kuwa na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi kuwataja wenye mahusiano nao ya kimapenzi ili watafutwe na kupimwa.

Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Salum Manyata, alitangaza mpango huo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani ambayo kimkoa yalifanyika katika Uwanja wa Barafu, Mji wa Lujewa, wilayani Mbarali.

Alisema lengo la mpango huo ni kudhibiti maambukizi mapya kwa maelezo kuwa mtu yeyote anayebainika kuwa na maambukizi anatakiwa kuanza kutumia dawa ili kupunguza uwezekano wa kuambukiza wengine.

Alisema yapo makundi yaliyo katika hatari ya kuambukizwa virusi hivyo na hivyo hao ndio huwa wanalengwa kwenye upimaji kwa kuwashawishi wakiwamo wanaotumia dawa za kulevya hasa kwa kujidunga.

"Ukishampima mtu akabainika kuwa ana maambukizi na akaingia kwenye matumizi ya dawa, unakuwa umekata ule mnyororo wa maambukizi na hivyo utaratibu huu unatusaidia kupunguza maambukizi mapya," alisema Dk. Manyata.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye alikuwa mgeni rasmi, aliwataka wadau wote wanaoshiriki kwenye mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU kukaa pamoja na kutunga sheria ndogo ambazo zitasaidia kwenye mapambano hayo kwa shuruti.

Alishauri kudhibiti maambukizi hayo kwa shuruti kwa kuwa kuna uwezekano kudhibiti kwa kutumia njia ya hiari imeshindikana kwa sababu inakuwa haina ulazima kwa mtu.

"Niwashauri ninyi wadau hasa wanasheria, halmashauri na nyie watu wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi, mkae pamoja mtunge By-Laws (Sheria ndogo), ambazo zitasaidia kudhibiti kwa shuruti tofauti na sasa ambapo tupo kwenye hiari," alisema Chalamila.

Alisema takwimu za maambukizi ya Ukimwi kwa Mkoa wa Mbeya ziko juu huku sababu halisi za tatizo hilo kuwa kubwa zikiwa hazijulikani vizuri na kushauri wataalamu waendelee kufanya utafiti.

Baadhi ya watu wanaoishi na VVU mkoani Mbeya, walieleza sababu za takwimu za maambukizi kuwa juu katika mkoa huo, ikilinganishwa na mikoa mingine, mmoja wa watu hao, Jenipher Makitunda, alisema tatizo kubwa la watu wanaoishi na VVU hawatulii katika kituo kimoja na badala yake wanahama kutoka sehemu moja kwenda nyingine.



# Mwinyi aonya visingizio ukusanyaji kodi

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amesema ugonjwa wa corona umekuwa kisingizio katika ukusanyaji wa kodi licha ya kwamba inaonyesha hakuna jitihada za makusudi kufikia lengo.

Akizungumza juzi Ikuku Zanzibar alipofanya mazungumzo na uongozi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ukiongozwa na Gavana Prof. Florens.

Alisema licha ya kuwapo kwa ugonjwa wa corona, mifumo ya kodi nayo ikikaa sawa mafanikio makubwa yanaweza kupatikana na kutekelezeka.

Dk. Mwinyi alisema uteuzi wa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango anayeshughulikia kodi na fedha, utasaidia na ni vyema kiongozi huyo akahakikisha katika muda mfupi mifumo inakaa sawa na kwa vile anatokea BoT ana matumaini makubwa kwamba atapata msaada kutoka benki hiyo.

Pia alisema uchumi wa Zanzibar kwa sasa unatilia mkazo katika uchumi wa bluu sambamba na utalii, uvuvi wa bahari kuu na sekta zingine, hivyo msaada wa kitaalamu wa kiuchumi utahitajika kwa kiasi kikubwa kutoka benki hiyo.

Dk. Mwinyi alisema kuna haja ya kutafuta njia bora ya kuwasaidia wajasiriamali ambapo mikopo inayotolewa hivi sasa masharti yake ni magumu ndiyo maana wengi wao wanafeli, hivyo msaada wa BOT unahitajika ili kupata njia nzuri zaidi.

Aliongeza kuwa licha ya kuwapo kwa bajeti ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ambayo inaonekana haukufanya vizuri kwa sababu mbalimbali ikiwamo dhana ya baadhi ya watu katika jamii kudhani kwamba fedha za serikali hutolewa kama zawadi, hivyo mrejesho wake huwa haukendi vyema.

Dk. Mwinyi aliihakikishia BoT ushirikiano wa serikali anayoiongoza ikiwa ni pamoja na kupokea ushauri kutoka benki hiyo kwa lengo la kuimarisha uchumi wa Zanzibar. Alisema upande wa Muungano uwezo mkubwa umejengwa sambamba na kufanya utafiti na matokeo yanaonekana na kueleza kwamba kwa upande wa Zanzibar nayo ina jukumu la kuyachukua na kuyafanyia kazi ili kuleta matokea chanya.

Alisema mifumo iliyojengwa kwa upande wa Tanzania Bara katika upande wa kodi, fedha, matumizi na mapato hivi sasa unakwenda vizuri na uwezo umejengwa kwa kutosha katika kuleta mafanikio hivyo azma ni kuungwa mkono. Naye Prof. Luoga alisema azma ya BOT ni kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuhakikisha uchumi wa Zanzibar unaimarika zaidi.

Alisema uchumi wa Zanzibar umeendelea kukua kwa kiwango cha kuridhisha kwa wastani wa asimilia 6.8 kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita na kwamba sekta ya huduma ndiyo imekuwa ikichangia zaidi.

Prof. Luoga alisema mwendo kasi wa mfumko wa bei umebakia tulivu na kasi ya mfumuko wa bei ilishuka kutoka tarakimu mbili mwaka 2011 ya asilimia 14.7 na kufikia tarakimu moja ya wastani wa asilimia 5.4 kwa kipindi cha mwaka 2013-2019.

Pamoja na mafanikio hayo, Prof. Luoga alisema bado kuna changamoto kadhaa ambazo Benki Kuu inaendelea kuzipatia ufumbuzi wa kudumu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Pia alisema pamoja na changamoto ya athari za corona, sekta ya kibenki imeendelea kuwa imara.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said (kushoto), akizungumza na Mwakilishi wa Mtandao wa Elimu (MINDZU), Khalaf Rashid, ofisini kwake Mazizini Mjini Unguja jana, kuhusu namna ya kuanza kufundisha masomo ya sayansi kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne kwa njia ya mtandao. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Madiwani CCM wafundwa utatuzi wa kero

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimewataka madiwani wake kuhakikisha wanatekeleza sera na ilani ya uchaguzi ya chama hicho, kwa kuwa mstari wa mbele kutatua kero zinazowakabili wananchi.

Katibu wa Kamati Maalum ya NEC, Idara ya Organization Zanzibar, Casian Galon Nyimbo, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na madiwani baada ya kumaliza uchaguzi Mwenyekiti wa Baraza la Mji Wilaya ya Kaskazini uliofanyika ofisi ya CCM, Mahonda.

Nyimbo alisema dhamana walizokabidhiwa madiwani hao ni kwa ajili ya kutatua kero za wananchi katika maeneo yao kwa kuzingatia kuwa wananchi wana matarajio makubwa kutokana na ahadi zilizotolewa na wagombea wa CCM ngazi mbalimbali wakati wa uchaguzi. Alisema dhamira ya CCM ni kuona ahadi za wagombea zinatekelezwa kwa ufanisi na kwa wakati ili wananchi wazidi kuwa na imani na chama hicho.

Naye Katibu wa CCM Wilaya ya Kaskazini B Unguja, Mwansiti Hassan Mohamed, aliwataka madiwani hao kuweka mbele maslahi ya chama badala ya binafsi na kuibua miradi itakayokuwa na manufaa kwa wananchi.

Mwenyekiti mpya wa Baraza la Mji Kaskazini B, Hassan Ameir Abdalla, aliahidi kushirikiana na viongozi wenzake katika kuwatumikia wananchi kwa mujibu wa matatizo walio nayo. Aliwataka madiwani wenye tabia ya kutoa siri za vikao kuacha mara moja kwa kuwa tabia hiyo haina maslahi kwa chama hasa wakati huu wa kuleta mageuzi ya kiuchumi.

# Makamu wa Rais awaonya vijana kuhusu Ukimwi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka vijana kukataa kuwa waathirika wa Virusi Vya Ukimwi (VVU), ili wabaki salama.

Akizungumza juzi katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani katika Ukumbi wa Sheikh Idris Abdulwakil, Kikwajuni, alisema bila kuwa na vijana wenye afya nzuri, wachapa kazi, dhamira ya serikali isemayo 'yajayo ni neema tupu' itabaki kuwa ndoto.

Alisema utafiti unaonyesha kuwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 24 bado wanaongoza katika kupata maambukizo mapya ya VVU kila mwaka kwa asilimia 50.

Hemed alisema mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU, yanahitaji ushiriki wa kila sekta kama ilivyojidhihirisha wakati wa mapambano dhidi ya corona. "Tumeshuhudia kuwapo kwa mashirikiano (ushirikiano) ya (wa) mataifa katika kukabiliana na corona yaliyoonyesha (ulioonyesha) kwamba taifa haliwezi kuwa salama kama taifa lingine haliko salama. Mshikamano huu pia unahitajika katika kumaliza virusi vya Ukimwi duniani," alisema.

Maeneo ya kazi kwa bahati mbaya, alisema bado yana viashiria vya kuwapo uwezekano wa watu kuambukizwa VVU, lakini juhudi za kuzuia maambukizo hayo haziendani na ukubwa wa viashiria, hivyo ni vyema ikawapo mipango itakayoyaweka maeneo hayo salama.

Aliwataka viongozi wa taasisi za serikali na za binafsi kutenga fedha kwa ajili ya kupambana na Ukimwi katika mipango ya kazi na kuhakikisha fedha hizo zinasimamiwa ili zitumike kwa lengo husika.

Pia alisema serikali ya Zanzibar kwa kushirikiana na washirika wake wa maendeleo, imepata mafanikio makubwa katika kupambana na maradhi hayo tokea yalipoingia nchini mwaka 1986 na kudhibitiwa kubakia kuwa chini ya asilimia moja.

Alisema pamoja na mafanikio hayo, bado ugonjwa huo ni tishio kwa taifa na kimataifa, hivyo jitihada zinatakiwa kuchukuliwa kupambana na mambo yanayozorotesha kasi ya serikali katika kupambana na janga hilo.

Hemed alisema uelewa finyu usioridhisha kwa baadhi ya wanajamii juu ya VVU umekuwa tatizo la kuenea kwa unyanyapaa ndani ya familia dhidi ya watu wanaoishi na virusi hivyo. Alisema utafiti unaonyesha kwamba asilimia 30.5 ya Wazanzibari 26.4 Unguja na 43.5 Pemba wana tabia ya unyanyapaa, tabia inayotakiwa kupigwa vita kwa nguvu zote ili lengo la kuondoa kabisa unyanyapaa kwa wanaoishi na virusi hivyo lifikie asilimia sifuri.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Shughuli za Baraza la Wawakilishi, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema wizara imekusudia kuandaa bajeti kwenye mpango wake wa mapambano dhidi ya VVU.

Dk. Khalid alisema jitihada kubwa zilizochukuliwa kati ya Tume ya Ukimwi Zanzibar kwa kushirikiana na Jumuiya ya Kupambana na Virusi vya Ukimwi Zanzibar (ZAPHA+), zimeiwezesha Zanzibar kupunguza maambukizi na kufikia zaidi ya asilimia 90 tatu zilizokusudiwa kimataifa.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:
- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam - 0768 928 516.**
**Arusha - 0677 226 960.**


*NIPASHE NI JIBU LAKO*
**NJOO UTANGAZE NASI**
**KWA BEI NAFUU SANA**
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**AMOSI MADINDA NGULUMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HILUX** yenye namba za usajili **T 132 AHL.Chassis No LN1070007731, Engine No.3L3060552.** Yeyote atakayeona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi DOD / DOD/RB/832902/2020.**

### KUPOTEA KWA CHETI



**TUNSUBILEGE JEREMIAH MWAIPOPO** ANATANGAZA KUPOTELEWA KWA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **CSEE P.1888/0029** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA SHULE YA **PATRICK MISSION HIGH** MWAKA **2017**,YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

**POLISI TAARIFA**
**WMB/RB/1137/2020**

### KUPOTEA KWA VYETI



**INNOCENT ZIRARIYE** ANATANGAZA KUPOTELEWA KWA VYETI,CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA **0631-0090** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI KUPITIA SHULE YA SECONDARY UMOJA MWAKA **2002**,CHA KIDATO CHA SITA INDEX NAMBA **S.0123-0534** SHULE YA SECONDARY KWIRO MWAKA **2005** NA CHETI CHA CHUO OPEN UNIVERSITY OF TANZANIA , BSC EDUCATION NAMBA **E.0003838** MWAKA **2011**,YEYOTE ATAKAYEVIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

**POLISI TAARIFA DAR/URA/RB/693257/2020**

**Appellate Jurisdiction**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT SONGEA**

**LAND APPEAL NO 8 / 2020**

(From the decision of the District Land and Housing Tribunal of Songea District in land Appeal/Application No 243 of 2016 And Original Ward Tribunal ward in Application No…….20….

**DR. WADE ASYUKILE KABUKA APPELLANT**

**VERSUS**

**ASUMAN RASHID AND 3 OTHERS RESPONDENTS**

**TO:………………………………………… ASUMAN RASHID**

**NOTICE OF DATE OF MENTION**

TAKE NOTES that the above case has been fixed for Mention on **16TH day of February 2021** at 09.00 a.m Before Hon I. Arufani JUDGE
You are required to appear in this Court on the fixed date without fail

Given under my hand and the seal of Court this
24th day of November of 2020

……………………………………
**DEPUTY REGISTRAR**

**TO BE SERVED UPON:**
**ASUMAN RASHID**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA**
**SENGEREMA**

**MADAI NO 08/2020**

**JOSEPH BOYA KACHILE……………………….MDAI**

**DHIDI YA**

1. **NATIONAL INSURANCE CORPORATION TANZANIA LTD..MDAIWA 1**
2. **JACOB KWIZE MTALITINYA……………MDAIWA 2**
3. **CHRISTOPHER STEVEN…………………MDAIWA 3**

Wewe **JACOB KWIZE MTALITINYA na CHRISTOPHER STEVEN** popote pale mlipo mnaamriwa na mahakama hii kuhudhuria hapa mahakamani mnamo tarehe 07/12/2020 kama hamtahudhuria basi mahakama hii itasikiliza upande mmoja na maamuzi kutolewa.

…………………………………
**HAKIMU MKAZI**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**SENGEREMA**

116025802




**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA TEMEKE**
**TEMEKE**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 297 YA 2020**
**PAMELA KOI WADAI/MDAI**
**DHIDI YA**
**N.M.B BANK P.L.C AND 4 OTHERS MDAIWA/ WADAIWA**
**KUITWA SHAURINI**
**DAR OIL CO LTD**
**ABDALLAH SILAJI**
**ANDREW T KOWELO**

**PAMELA KOI** amefungua shauri mbele ya baraza la ardhi na nyumba lililopo temeke usalama. Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe **07/12/2020** mbele ya mhe **J.M.BIGAMBO** hivyo basi mnatakiwa/ unatakiwa kuleta utetezi wenu/wako ndani ya siku **21** kuanzia tarehe ya tangazo hili kutolewa . vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika masjala ya wazi baraza la ardhi na nyumba ya temeke. Endapo hautatekeleza haya shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa .
Amri hii imetolewa na kutiwa sain na mhuri wa baraza leo hii tarehe **11/11/2020**


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI**
**INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB:**
**+255 - 0782253676**



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Wafariki kwa kugongwa na gari, 10 wajeruhiwa

**TRIER,** Ujerumani

WATU wawili wamefariki dunia, na wengine 10 kujeruhiwa baada ya kugongwa na gari katika njia ya watembea kwa miguu katika mji wa Trier, Jimbo la Rhineland-Palatinate nchini Ujerumani.

Taarifa iliyotolewa na Jeshi la Polisi katika mji wa Trier walieleza kuwa gari hilo lililoingia katika barabara ya wapita njia, liligonga na kuwajeruhi watu wengi.

Kulingana na taarifa za Shirika la SWR linalohusiana na Kituo cha Televisheni cha Kwanza cha Ujerumani ARD, iliarifiwa kuwa watu wawili walifariki na wengine 10 walijeruhiwa katika tukio hilo.

Taarifa zaidi zimebainisha kuwa dereva wa gari hilo alikamatwa. **TRT**

## Uingereza ya kwanza kuidhinisha chanjo corona

**LONDON,** Uingereza

UINGEREZA imekuwa nchi ya kwanza duniani, kuidhinisha matumizi ya chanjo dhidi ya ugonjwa wa virusi vya corona iliyotengenezwa na maabara ya Marekani ya Pfizer na mshirika wake BioNTech kutoka Ujerumani.

Chanjo hiyo itapatikana nchi nzima kuanzia wiki ijayo, serikali ya Uingereza ilisema jana katika taarifa.

Matumizi hayo yameidhinishwa na Mamlaka ya Dawa Uingereza, (MHRA). Hadi sasa hakuna chanjo yoyote ambayo imeidhinishwa katika nchi yoyote duniani. **RFI**

## Wanafunzi huambukizwa VVU kwa wingi

**NAIROBI,** Kenya

ENEO la Kanda ya Ziwa, nchini Kenya linaongoza kwa idadi ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU).

Kwa mwaka huu pekee watu 20,000 walifariki kwa Ukimwi, kati ya vifo hivyo vingi ni wanaume.

Wakati jana ikiwa ni Siku ya Ukimwi Duniani, takwimu za Kenya zimeonyesha kuwa wanafunzi ndiyo wanaambukizwa VVU kwa wingi, wengi wao ni wasichana.

Uwapo wa ugonjwa wa virusi vya corona umezua utata mpya kwa kuwa dawa za kupambana na makali ya VVU zimekuwa adimu. **DW**

# Bobi Wine aahirisha kampeni zake za urais

**KAMPALA,** Uganda

MGOMBEA urais Uganda, Robert Kyagulanyi, maarufu kama Bobi Wine, ameahirisha kampeni zake, kufuatia kujeruhiwa kwa maofisa wake na kuharibiwa kwa gari lake.

Kiongozi huyo wa upinzani alisema risasi zilifyatuliwa kwenye gari lake na kutoboa matairi na kumsababisha kutoendelea na safari.

Video zilizosambazwa na timu yake ya kampeni kwenye mitandao ya kijamii, zinaonyesha kitu ambacho hakikutambuliwa kikilipuka umbali wa mita kadhaa kutoka mahali alipokuwa.

**Awali katika eneo la Kayunga, mashariki mwa Kampala, mabomu ya kutoa machozi yalitumika kuwatawanya wafuasi wake.**

Awali katika eneo la Kayunga, mashariki mwa Kampala, mabomu ya kutoa machozi yalitumika kuwatawanya wafuasi wake. Maofisa wanne wa kampeni yake walijeruhiwa.

Mmoja wao, aliyetambuliwa kama producer Dan Magic alipigwa usoni, vilevile mmoja wa polisi wanaowalinda wagombea wa urais waliotolewa na Tume ya Uchaguzi naye alijeruhiwa.

Takriban wiki mbili zilizopita, watu 54 waliuawa wakati wafuasi wa mgombea huyo walipokuwa wakiandamana kudai aachiliwe huru, baada ya kukamatwa na polisi katika mkutano wa kampeni.

Baadaye alishtakiwa kwa kukiuka masharti ya kukabiliana na janga la corona kwa kukusanya umati wa watu, lakini baadaye aliachiliwa kwa dhamana. Vikosi vya usalama vimeendelea kuzuwia mikutano yake ya kisiasa pamoja na ya wanasiasa wengine wa upinzani.

Katika hotuba yake ya kitaifa Jumapili, Rais Yoweri Museveni, aliwatetea polisi na jeshi akisema kuwa hakuna mwanasiasa yoyote ambaye hawezi kuguswa. **BBC**



Wanaharakati kutoka Jiji la Hong Kong China, Joshua Wong (kulia), Ivan Lam (katikati), Agnes Chow, ambao wamehukumiwa kifungo jela kwa kosa la kushiriki maandamano ya kudai demokrasia. **PICHA: AFP**

# Mwanasheria Mkuu: Hakuna ushahidi wizi wa kura Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

MWANASHERIA Mkuu wa Marekani, William Barr, amesema Wizara ya Sheria imechunguza madai ya udanganyifu katika uchaguzi mkuu wa urais uliofanyika Novemba 3, mwaka huu, haijapata ushahidi kuthibitisha madai yaliyotolewa na Rais Donald Trump.

Alisema madai yaliyotolewa na timu ya kampeni na kisheria ya Rais Trump kwamba uchaguzi ulighubikwa na wizi wa kura, hadi sasa hawajapata ushahidi wowote kuhusu udanganyifu katika kiwango ambacho kinaweza kuyaathiri matokeo yaliyompa ushindi Joe Biden.

Matamshi hayo yanaonekana kama pigo kubwa kwa Rais Trump, ambaye hajakubali kushindwa.

Barr alisema kwamba kumekuwa na madai kuhusu udanganyifu wa kimfumo na kwamba mashine zilipangwa mahsusi kwa ajili ya kuchakachua matokeo ya urais.

Kwa muda mrefu Barr amekuwa akionekana kuwa mtiifu kwa Rais Trump tangu alipochukua nafasi ya Jeff Sessions mwaka 2018.

Kabla ya uchaguzi vyombo vya habari viliripoti kuhusu Rais Trump kutoridhishwa na mwenendo wake, kwamba hakuonesha juhudi katika harakati za kiongozi huyo kuchaguliwa tena kuiongoza Marekani.

Barr aliamuru uchunguzi ufanyike mwezi uliopita na aliwaamuru waendesha mashtaka wa shirikisho kuchunguza madai yoyote ya kuaminika ya udanganyifu. **DW**

## HABARI MICHEZO

# ARSENAL, TOTTENHAM ZOTE KWA SZOBOSZLAI




**LONDON,** England

TIMU za Arsenal na Tottenham Hotspur zimeripotiwa zipo kwenye mbio moja za kuwania saini ya nyota wa Salzburg, Dominik Szoboszlai.

Szoboszlai mwenye umri wa miaka 20, amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kutoka Salzburg baada ya kung'ara kwenye klabu hiyo ya nchini Austria.

Huku pia klabu nyingine saba kubwa za Ulaya zikiwa pia zinamkodolea macho mchezaji huyo wa kimataifa wa Hungary, Arsenal na Tottenham tayari zimeonyesha kuongoza kwenye mbio za kuwania saini hiyo ya nyota huyo wa Salzburg, Szoboszlai, kwa mujibu wa Eurosport.

Lakini ripoti zaidi zinaeleza kuwa, RB Leipzig inaonekana kuwa na nafasi nzuri zaidi ya kushinda kwenye mbio za kuwania saini ya nyota huyo.

Klabu za AC Milan na Atletico Madrid nazo zimeripotiwa kuwa na nia ya kuiwania saini ya mchezaji huyo.

Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo unamalizika mwaka 2022, na thamani yake inatajwa kuwa ni euro milioni 20.

# Simeone alia na umaliziaji Atletico

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone anatambua kwamba kushindwa kutumia nafasi walizozipata kumeigharimu Atletico Madrid, baada ya kikosi chake hicho kutoka sare ya kufungana bao 1-1 na Bayern Munich.

Atletico walikwenda kwenye mchezo huo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya Jumanne dhidi ya bingwa huyo mtetezi Bayern wakijua kwamba ushindi ungetosha kuwapa nafasi ya pili kwenye Kundi A.

Joao Felix aliwapa Atletico bao la uongozi likiwa ni la nane katika mechi 14 msimu huu, lakini wenyeji hao walishindwa kufunga tena licha ya kupata nafasi 12, huku tatu tu ndio zilkilenga goli.

Bayern ambayo ilikuwa bila ya nyota wake, Robert Lewandowski na Manuel Neuer, walisawazisha bao hilo kwa mkwaju wa penalti dakika ya 86 ikifungwa na Thomas Muller.

Hiyo sasa inamaanisha kwamba, Atletico wanahitaji kutofungwa na Salzburg kwenye mchezo wao wa mwisho wa kundi hilo, ili iweze kufuzu hatua ya mtoano, na Simeone anajua vizuri wapi panapohitajika kikosi chake kuimarika.

"Hatukuwa na nguvu sana kwenye mashambulizi, lakini tulitengeneza nafasi," alisema Simeone akiiambia Movistar Plus. "Sasa tuna mchezo mgumu sana dhidi ya Salzburg.

"Ukifunga mabao machache maana yake mara zote unaweza kukamatwa. Lakini hadi penalti Bayern haikuwa na nafasi ya kufunga."






# *Queiroz ajiuzulu ukocha Colombia*

**BOGOTA,** Colombia

CARLOS Queiroz ameachia nafasi yake kama kocha mkuu wa timu ya Taifa ya Colombia ikiwa ni karibu ya miaka miwili.

Kuondoka kwa Queiroz kulitangazwa na Shirikisho la Soka la Colombia (FCF), Jumanne baada ya timu hiyo kuwa na mwanzo wa taratibu kwenye kufuzu michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2022.

Colombia, ambayo ilishiriki kwenye michuano miwili ya Kombe la Dunia iliyopita, imeshinda mchezo mmoja tu kati ya minne za kufuzu na ina pointi nne na ipo nafasi ya saba kwenye kundi lake.

"Shirikisho la Soka la Colombia na Mkurugenzi wa soka, tumekubaliana kwamba, Carlos Queiroz hataendelea na majukumu yake ya kuwa kocha mkuu wa timu ya taifa ya wanaume," ilisomeka taarifa hiyo.

Kocha huyo wa zamani wa Real Madrid, Ureno na Iran, Queiroz alichukua mikoba ya kuinoa Colombia Februari mwaka jana. Aliiongoza kwenye mechi 18, akishinda tisa, sare tano na kupoteza nne.

Lakini Colombia ilipoteza kwa mabao 3-0 kwa Uruguay na kafumuliwa 6-1 na Ecuador kwenye michuano hiyo ya kufuzu mwezi uliopita, na ndiyo sababu ya kuachia ngazi.

## HABARI MICHEZO

# Guardiola: Foden ni bonge la mchezaji

**LONDON,** England

PEP Guardiola amemmwagia sifa, Phil Foden kwa kuonyesha kiwango bora zaidi wakati Manchester City ikitoka sare ya bila kufungana na Porto kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

City walionekana kuwa kwenye wakati mgumu katika mchezo huo uliopigwa pale katika dimba la Estadio do Dragao, huku bao la Gabriel Jesus likikataliwa na VAR kwa kuwa alikuwa ameotea katika dakika ya 10.

Hata hivyo, sare hiyo iliwawezesha miamba hao wa Ligi Kuu England kupaa kileleni mwa Kundi C.

Foden ameanza katika mechi nne mfululizo za Ligi ya Mabingwa Ulaya, ingawa kiungo huyo wa kimataifa wa England ameanzia benchi kwenye mechi tano za City zilizopita za ligi ya nyumbani.

Akizungumza na BT Sport, Guardiola alionekana kutambua kiwango cha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, na kwamba amekuwa akianza mara kwa mara kwenye kikosi cha kwanza kwenye mashindano hayo.

"Ni mchezaji wa aina yake," alisema wakati alipoulizwa kuhusu kiwango cha Foden.

"Ana ubora na mara zote anatengeneza vitu. Alikuwa mzuri sana, nimefurahishwa na kiwango chake."

Foden alitengeneza pasi muhimu mbili na pia pasi zilizokamilika nne kwa kikosi hicho cha City.





# KLOPP AJISIFU KUIFUNGA AJAX

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amejisifu kuwa na moja ya usiku mkubwa zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kama kocha wa Liverpool, baada ya 'Wekundu' hao kufuzu hatua ya mtoano kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ajax.

Liverpool walikuwa hawajashinda katika mechi zake mbili zilizopita, huku wakikabiliwa na majeruhi wengi - walipata pointi hizo tatu muhimu Jumanne, shukrani kwa bao la Curtis Jones la kipindi cha pili.

Jones alikuwa mchezaji wa tatu mwenye umri mdogo zaidi kuifungia Liverpool kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya David N'Gog mwaka 2008 na Trent Alexander-Arnold mwaka 2017.

Ushindi huo ulikuwa mzuri zaidi kwao, baada ya Atalanta kutoka sare na Midtjylland nchini Italia, na hivyo kuwawezesha mabingwa hao wa Ligi Kuu England kukaa kileleni mwa Kundi D.

Huku akiwa hajashinda katika mechi mbili zilizopita, ushindi huo ulikuwa furaha kubwa kwa Klopp.

"Inaonyesha kama moja ya usiku mkubwa sana kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya tuliokuwa nao; bila mashabiki, lakini ilikuwa ni muhimu sana kushinda katika mchezo huu wa aina yake," alisema Klopp akiiambia BT Sport.

"Mazingira yalionekana kuwa magumu, lakini jambo zuri ni kwamba, tulipigana kuhakikisha tunapambana na kupata ushindi, hasa ikizingatiwa ukweli kuwa tuna majeruhi wengi."

# *Conte matumaini kibao kwa Inter*

**DORTMUND,** Ujerumani

ANTONIO Conte amesifia morali ya Inter Milan wakati wakiweka hai matumaini ya kupata nafasi ya kufuzu hatua ya mtoano kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kushinda kwa mabao 3-2 ugenini dhidi ya Borussia Monchengladbach.

Inter ilikuwa na wakati mzuri baada ya kushindwa kushinda mechi zake nne za Kundi B kwenye Ligi ya Mabingwa, na sasa wanahitaji ushindi kwenye mchezo mmoja uliobaki ili kufuzu hatua ya mtoano.

Matteo Darmian aliiweka mbele Inter kabla ya Alassane Plea kusawazisha kabla ya kipindi cha pili.

Halafu Lukaku akafunga mawili mazuri na kuwaweka Inter mbele kwa mabao 3-1 na licha ya Plea kufunga bao la pili zikiwa zimebaki dakika 15 mchezo kumalizika, halikutosha kuwanyima ushindi Inter.

Sasa wanahitaji kuifunga Shakhtar Donetsk na kuwaombea Gladbach washinde dhidi ya Real Madrid, ambao walifungwa kwa mara ya pili msimu huu na miamba hao wa Ukraine.

Inter walionekana kuwa kwenye kiwango kizuri cha kutafuta ushindi katika mchezo huo, wakipiga mashuti 15 langoni mwa Gladbach waliokuwa na mashuti 10, na Conte alibainisha ari ilivyowabeba.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MODRIC: MADRID INA WAKATI MGUMU UEFA

## ●●● Ni hali ngumu sana, bado tuna mchezo mmoja umebaki na tutakwenda kujaribu...

**KIEV,** Ukraine

LUKA Modric anatambua Real Madrid ipo "kwenye hali ngumu sana" huku matumaini yao katika Ligi ya Mabingwa Ulaya yakiwa hafifu baada ya kupokea kichapo kingine kutoka kwa Shakhtar Donetsk.

**Madrid ilifungwa mabao 2-0 na Shakhtar juzi, Jumanne matokeo ambayo yamewaacha mabingwa hao wa LaLiga katika na fasi ya tatu kwenye Kundi B na inakabiliwa na uwezekano wa kutolewa kuelekea mechi za mwisho za makundi.**

Wakiwa wametoka kufungwa na Deportivo Alaves kwenye LaLiga Jumamosi, Madrid ikakumbana na kipigo cha pili mfululizo, kwa mabao ya Dentinho na Manor Solomon pale mjini Kiev.

Madrid sasa imeruhusu nyavu zake kutikiswa mara tisa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu, ikionyesha kwamba wana safu ya ulinzi ya ovyo zaidi katika historia yao ya mashindano hayo hatua ya makundi.

Kikosi hicho cha kocha, Zinedine Zidane kilipoteza nyumbani kwa Shakhtar na sasa kina pointi sawa na wapinzani wake hao, huku kikipitwa pointi moja na vinara Borussia Monchengladbach na wakiwazidi pointi mbili Inter Milan inayoshika mkia kwenye kundi hilo.

Akiangalia matokeo hayo, kiungo Modric alisema: "Ni ngumu kuelezea baada ya kipindi cha kwanza sisi kucheza vizuri na kutengeneza nafasi chache, lakini hatukuweza kufunga mabao.

"Katika kipindi cha pili, baada ya wao kufunga, kila kitu kilibadilika na tulianza kucheza mchezo mwingine kabisa. Tulianza kuwa waoga uwanjani. Ni ngumu kuelezea.

"Ni hali ngumu sana, lakini hivyo ndivyo ilivyo. Bado tuna mchezo mmoja umebaki na tutakwenda kufanya kila kitu kujaribu kushinda mchezo huo, ambao kwetu utakuwa na umuhimu mkubwa sana."

Aliongeza: "Tulishindwa kucheza kwa kiwango chetu kama ilivyo kila siku. Tulikuwa na moja ya mchezo wa aina yake, mechi mbili mbaya, mmoja mzuri, mbili mbaya... hivyo ndivyo ilivyo.

"Tulishindwa kuwa kwenye kiwango chetu na tunatakiwa kuimarika haraka inavyowezekana."

## ZISIKUPITE

### WHITE AZIVUTA UTD, CHELSEA

MANCHESTER United na Chelsea zinamfuatilia kwa karibu mlinzi wa Brighton, Ben White, 23, ambaye thamani yake inatajwa kuwa juu sana. ***(Sky Sports)***

### BARCA KWA MUSTAFI, RUDIGER

BARCELONA wanafuatilia upatikanaji wa kiungo wa kati wa Arsenal, Shkodran Mustafi , 28, na mlinzi wa Chelsea, Antonio Rudiger, 27, huku wachezaji hao hawatakiwi na klabu zao. ***(Mundo Deportivo)***

### SZOBOSZLAI SASA LULU ULAYA

ARSENAL na Tottenham ni miongoni mwa klabu kadhaa zenye nia ya kumsaini kiungo wa kati wa Red Bull Salzburg, Dominik Szoboszlai , 20, huku RB Leipzig, AC Milan na Atletico Madrid pia zikionyesha nia ya kumtaka mchezaji huyo wa Hungary. ***(Eurosport)***

### ZAKARIA AGOMBEWA EPL

MANCHESTER United, Manchester City na Chelsea wapo kwenye mbio moja kuwania kumsajili kiungo wa kati wa Borussia Monchengladbach na Uswisi, Denis Zakaria, 24, wakati wa dirisha dogo la Januari. ***(Star)***

### SPURS BADO KWA SKRINIAR

KLABU ya Tottenham Hotspur bado inataka kumsajili mlinzi wa Inter Milan na Slovakia, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 25, licha ya mazungumzo kati ya klabu hizo kuvunjika msimu uliopita. ***(Football Insider)***

### ONANA ANA NAFASI EPL

GOLIKIPA wa Ajax na Cameroon, Andre Onana , 24, anaweza bado kufanikiwa kuhamia katika klabu ya Ligi Kuu ya England msimu ujao, baada ya Tottenham na Chelsea kujitoa kumwania. ***(Mail)***

### BUENDIA HUYO ARSENAL

ARSENAL bado hawajaweka dau la kiungo wa kati wa Norwich, Emi Buendia mwenye umri wa miaka 23, huku raia huyo wa Argentina akiwa miongoni mwa wachezaji wanaoweza kutia saini kwa 'Washikabunduki' hao wa London. ***(Football London)***

### VIEIRA AMTAKA SALIBA

KIUNGO wa zamani wa Arsenal, Patrick Vieira, ambaye kwa sasa ni kocha wa Klabu ya Nice ya Ufaransa, anataka kumpeleka klabuni hapo mchezaji William Saliba mwenye umri wa miaka 19. ***(Metro)***

### JUVE KWA EMERSON, GIROUD

JUVENTUS wanajiandaa kuongeza maradufu dau lao kwa ajili ya kuwawania nyota wa Chelsea, Emerson Palmeri mwenye umri wa miaka 26 na Olivier Giroud, 34. ***(Il Bianco Nero)***

### BARCA KUMCHUKUA AUGUSTO

BARCELONA wamechagua mlinzi wa Atletico Madrid na Brazil, Felipe Augusto mwenye umri wa miaka 31, kama mchezaji wao mbadala wa kuchukua nafasi ya Gerard Pique mwenye miaka 33, ambaye ni majeruhi, kwa ajili ya kumalizia msimu huu. ***(AS)***

# MABADILIKO YANGA YAELEKEA PATAMU

**Na Saada Akida**

MCHAKATO wa mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji katika klabu ya Yanga unaelekea patamu baada ya Mwenyekiti wao, Dk. Mshindo Msolla, kukabidhiwa ripoti ya rasimu ya awali ambayo imefanyiwa kazi nchini Hispania.

Mabakidhiano hayo yalifanyika jijini Dar es Salaam, jana, baada ya Kamati ya Mabadiliko iliyoko chini ya Mwenyekiti, Alex Mgongolwa, Mkurugenzi Mwezeshaji wa GSM, Hersi Said na Mshauri wa klabu hiyo, Senzo Mazingisa, kurejea kutoka Hispania ambapo walienda kuiandaa kwa ushirikiano na mabosi wa LaLiga.

Akizungumza jijini jana, Dk. Msolla alisema amepokea ripoti hiyo na ameikabidhi kwa Senzo kwa ajili ya kuanza mchakato wa hatua ya kwanza.

Msolla alisema wamemkabidhi Senzo kwa sababu ndiye mwenye jukumu la kusimamia mchakato huo kutoka kwenye mfumo wa zamani wa umiliki wa wanachama kuelekea katika uendeshaji wa kisasa wa kumiliki hisa.

"Ripoti tumeipokea na ni yenye kurasa takriban 403 ambapo itapitiwa na Kamati ya Utendaji ikishirikana na Kamati ya Mabadiliko na Kamati ya Sheria kabla ya kupelekwa kwa wanachama kupitia matawi ili kuwashirikisha wadau wote nchi nzima.

**"Wanachama na mashabiki wasiwe na wasiwasi juu ya mchakato huu kwa sababu klabu itabaki kuwa yao," alisema Msolla.**

Aliongeza kabla ya hatua hiyo, wataunda kamati ndogo kwa ajili ya kwenda katika mchakato wa mabadiliko ya katiba kulingana na mapendekezo ya ripoti hiyo waliyoipokea.

"Tunaahidi kufuata taratibu zote ikiwamo mwongozo wa serikali kukamilisha mchakato huu ambao ulikuwa ni ilani yangu ya kwanza nilipokuwa katika kampeni ya uchaguzi mwaka jana," alisema Msolla.

Naye Mgongolwa, alisema mabadiliko hayo yamejikita kuendesha klabu hiyo kwa mfumo wa kisasa kwa kuwajali mashabiki na wanachama wa klabu hiyo.

"Awali tulichaguliwa kamati ambayo niliiongoza, lakini baadaye tukapata mshirika ambaye ni LaLiga kwa lengo la kuunda timu kwa ajili ya kushirikiana katika mchakato huu," alisema Mgongolwa.

## NI TIKI-TAKA J'MOSI...




Ofisa Habari wa Simba, Haji Manara, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, kuhusu mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Plateau United ya Nigeria utakaopigwa Jumamosi ijayo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, ambao ametambulisha kuwa wataonyesha 'tik-taka' na kuvuna ushindi wa kishindo. Kushoto ni Mwenyekiti wa klabu hiyo, Mwina Kaduguda. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Azam FC yamkana Lwandamina*

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Azam imekanusha kufanya mazungumzo na makocha mbalimbali ambao waliwahi kufanya kazi hapa nchini, wakiwamo Mzambia George Lwandamina, Mkongomani Mwinyi Zahera, waliowahi kuifundisha Yanga na Thierry Hitimana aliyeachana na Namungo FC hivi karibuni.

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia, alisema jana si kweli klabu yao inaendelea na mazungumzo na makocha hao wa kigeni waliowahi kufundisha soka hapa nchini, lakini alieleza wanaendelea kusaka mwalimu kwa umakini na siri ili kufanikisha mahitaji yao.

"Habari au tetesi hizo hazina ukweli wowote, ukweli ni Azam FC iko kwenye mchakato wa kumpata kocha mkuu unaofanywa kwa umakini mkubwa na siri kubwa.

"Hivi ninavyokwambia mimi mwenyewe sijui. Mchakato unasimamiwa na wakubwa, sisi tutaambiwa tu ukikamilika, tutapata taarifa za mwisho ndio tutawatangazia mashabiki wetu na Watanzania kwa ujumla," alisema Zacharia.

Aliwatoa hofu mashabiki wa timu hiyo kwa kuwaambia wanataka kupata kocha mwenye uwezo wa hali ya juu ambaye ataitoa timu hiyo hapo na kuipeleka sehemu nyingine ya mafanikio.

"Mashabiki waendelee kusubiri, mchakato unaendelea, ni lazima tupate kocha mzuri. Unajua si tu uwe na gari zuri, lakini pia ni lazima uwe na dereva bora. Mchakato unaofanyika sasa ni wa kupata dereva mzuri ili gari na dereva vyote viwe vinafanana," Zacharia alisema.

Kwa sasa kikosi cha Azam kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya mechi inayofuata ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Gwambina FC itakayochezwa Jumatatu jijini Mwanza.

## Kipanga yatakata Ligi Kuu Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Kipanga imeendelea kufanya vizuri baada ya kuifunga Mlandege bao 1-0 katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan visiwani hapa, juzi jioni.

Kwa matokeo hayo, Kipanga imefikisha pointi saba na kujiweka kwenye mazingira mazuri katika msimamo wa ligi hiyo.

Bao pekee katika mchezo huo lilifungwa na Rajab Is-haka 'Morrison' dakika ya 46 baada ya kufyatua kombora safi lililomshinda mlinda mlango wa Mlandege.

Akizungumza na gazeti hili, Kocha Mkuu wa Kipanga, Rashid Lato alisema ushindi walioupata katika mechi hiyo umetokana na kuyafanyia kazi makosa waliyoyabaini katika mchezo uliopita.

Lato alisema wachezaji wake walicheza vizuri katika vipindi vyote viwili licha ya wapinzani wao kupambana, lakini hawakuwa na bahati ya kufunga katika mechi hiyo.

"Tumecheza vizuri, wachezaji wanastahili pongezi, lakini wapinzani wetu pia walicheza vizuri, mchezo ulikuwa mgumu sana kwa sababu hakuna timu inayotaka kupoteza au kutoa sare, kila moja lengo lake ni kupata alama tatu uwanjani," alisema Lato.

Kipanga ilianza msimu wa Ligi Kuu Zanzibar kwa sare ya bao 1-1 dhidi ya JKU na mechi iliyopita ilipata ushindi mnono wa mabao 3-0 dhidi ya Hard Rock.

Mzunguko wa tatu wa Ligi Kuu Zanzibar utaendelea kwa KMKM kushuka Uwanja wa Mau A dhidi ya Mafunzo.

## Ihefu yasisitiza itazinduka Bara

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Ihefu FC ya Mbarali jijini Mbeya, Zuberi Katwila, amewaahidi mashabiki na wanachama wa timu hiyo watarajie kupata matokeo mazuri baada ya kuanza kwa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katwila alisema tayari ameshaandaa ripoti ya kiufundi kuelekea katika kipindi cha usajili wa wachezaji wa dirisha dogo na anaamini utekelezaji wake ndio utaiondoa timu hiyo 'mkiani'.

Katwila alisema wachezaji atakaowaongeza katika kikosi chake watakuwa na uwezo wa kuipa timu hiyo matokeo mazuri na hatimaye kujinusuru na janga la kushuka daraja.

"Tayari nimeshaandaa ripoti kwa kuzingatia upungufu uliopo katika kila idara, tutakapofanikiwa kupata wachezaji wengine wenye uzoefu, ninaamini tutatoka hapa tulipo, kila mmoja ana malengo yake na anapambana kuyafikia," alisema Katwila.

Aliongeza ligi bado ni ngumu na ushindani unaongezeka kila wanapocheza, kila timu haitaki kupoteza pointi iwe nyumbani au ugenini.

# Michezo

Alhamisi Desemba 3, 2020

Nipashe




Modric: Madrid ina wakati mgumu UEFA UKURASA 22

# SIMBA YAJA NA TIKI-TAKA KWA MKAPA

## ●●● Yasema Plateau watakiona Jumamosi, Talib Hilal aionya asema...

**Na Saada Akida**

HUKU ikimtambulisha kiungo mpya Taddeo Lwanga kutoka Klabu ya Tanta ya Ligi Kuu Misri na timu ya Taifa ya Uganda, uongozi wa Klabu ya Simba umesema kamwe hautawadharau wapinzani wao kwenye mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Plateau United kutoka Nigeria licha ya mechi ya awali kushinda bao 1-0 ugenini.

**Aidha, Simba ambayo itarudiana na Wanigeria hao Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es-Salaam, imesema lengo lao ni kuingia uwanjani kupambana mwanzo mwisho ikisaka ushindi wa kishindo sambamba na kuonyesha 'Tiki-taka' kwa mashabiki wao na wapenzi wa soka nchini kwa ujumla.**

Tiki-Taka ama ['Tiqui-Taca'] ni staili ya Kihispania ya uchezaji soka la pasi fupi na kupenyeza mpira katika nafasi mbalimbali likienda sambamba na kumiliki zaidi mpira.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini jana, Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, Mwina Kaduguda, alisema wanajipanga kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo huo wa maruadiano ili kuvuka hatua hiyo ya awali na endapo wataibuka na ushindi, Simba watacheza na mshindi wa jumla kati Costa do Sol ya Msumbiji ama FC Platinum ya Zimbabwe ambayo nayo ilipata ushindi wa mabao 2-1 katika mechi ya awali ugenini.

Alisema hii ni mara ya kwanza kwa timu kutoka Tanzania kushinda ugenini katika ardhi ya Nigeria, hivyo wanahitaji kupambana dakika 90 zingine kutafuta ushindi, ili kufikia malengo yao ya kusonga mbele ya michuano hiyo na kufika nusu fainali.

"Hatutabweteka, mimi najua mpira wale jamaa ni wazuri, tunatakiwa kupambana dakika 90, tunafanya jitihada za kuhakikisha hawatoki katika uwanjani wetu wa nyumbani. "Hatusikilizi propaganda kwamba wapinzani wetu ni wa kawaida maana ni mabingwa wa Nigeria tukumbuke amemfunga Enyimba ambaye ni mabingwa mara tatu, kila mmoja anajua ubora wa Enyimba," alisema Kaduguda.

Kaduguda pia hakusita kuipongeza Bodi ya Wakurugenzi wa Simba chini ya Mwenyekiti wao, Mohamed 'Mo' Dewji, kwa kujitolea kusaidia klabu hiyo hasa katika kipindi hiki cha mchakato wa mabadiliko.

Alisema Mo Dewji amefanikiwa kutoa Sh. milioni 700 kuhakikisha anamwongeza mkataba Clatous Chama kuendelea ili kubaki ndani ya klabu hiyo.

"Ukimtoa Chama, hivi leo (jana) tumetambulisha nyota mpya Mganda Taddeo Lwanga ambaye anakuja kuchukuwa nafasi ya Gerson Fraga," alisema Kaduguda.

Wakati huo huo, Ofisa Habari wa Simba, Hajji Manara, alisema msimu huu wanakuja na kauli mbiu ya 'Tiki-Taka kwa Mkapa', ambayo italenga si kupata ushindi tu bali pia kutoa burudani kwa mashabiki na Watanzania kwa ujumla.

"Hii maana yake si kushinda tu, bali kutoa burudani kwa Watanzania na kuwafundisha soka wapinzani wetu, pia tukumbuke kwa Mkapa ni 'machinjio' ya wageni wetu. Hii ni mechi yetu, tunatakiwa kujaza uwanja kwa wingi tena iwe nyeupe na nyekundu, kwa sababu tunaenda kumuenzi, Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamini Mkapa kwa kutafuta ushindi maana sisi ni klabu ya kwanza kucheza mechi ya kimataifa hapa tangu ubadilishwe jina kutoka Uwanja wa Taifa," alisema Manara.

Aidha, alisema wageni wao, Plateau United wanatarajiwa kuwasili nchini Ijumaa, huku waamuzi wa mchezo huo kutoka Kenya wakitarajiwa kuwasili leo, na viingilio vya mchezo huo akivitaja kuwa ni Sh. 150,000 kwa Platinum, Sh. 40,000 VIP A, Sh. 30,000 VIP B na C huku mzunguko ikiwa buku saba tu.

Katika hatua nyingine, aliyekuwa Kocha wa Simba, Talib Hilal amewataka wachezaji wa timu yake hiyo kusahau mechi iliyopita na kushuka dimbani Jumamosi kwa tahadhari kubwa kwa kuwa kwenye soka lolote linaweza kutokea na kubadilisha matokeo ya awali.

Akizungumza na gazeti hili kwa simu kutoka Oman, Talib ambaye ni mkufunzi wa soka la ufukweni nchini humo, alisema: "Nigeria watakuja kwa lengo moja tu kushinda, kwa hiyo watacheza soka la kushambulia, lazima Simba wacheze kwa tahadhari na kusahau matokeo ya mechi ya kwanza.

"Kuna ugonjwa wa kuridhika, tunapopata ushindi, sasa tunatakiwa kujifunza ya msimu uliipita tulitoka sare dhidi ya UD Songo ya Msumbiji kwao na walipokuja nyumbani walituondoa katika hatua ya awali."

JEMBE...



Mwenyekiti wa Klabu ya Simba, Mwina Kaduguda (kushoto), akimtambulisha kiungo mpya wa timu hiyo, Mganda Taddeo Lwanga, aliyejiunga na mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara akitokea Klabu ya Tanta ya Ligi Kuu Misri. **PICHA: SIMBA**

# Ngorongoro yavuliwa ubingwa CECAFA U-20

**Na Mwandishi Wetu,** KARATU

IKICHEZA mbele ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, timu ya Soka ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), imevuliwa ubingwa wa mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-20), baada ya kukubali kichapo cha mabao 4-1 katika mechi ya fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Black Rhino Academy mjini Karatu jana.

Yosso hao wa Uganda wamelipa kisasi cha kuubeba ubingwa huo baada ya mwaka jana Ngorongoro Heroes kuwafunga wakiwa nyumbani kwao katika Mji wa Jinja, Uganda. Hata hivyo mabingwa Uganda pamoja na Ngorongoro Heroes wote wamefuzu kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa vijana U-20 zitakazofanyika nchini Mauritania mwakani.

Uganda walikuwa wa kwanza kupata bao dakika ya 12 kupitia kwa Richard Basangwa na Ngorongoro Heroes walisawazisha kwa penalti iliyopigwa na Abdul Hamisi dakika ya 30, lakini Steven Sserwadda aliwapatia wageni hao goli la pili dakika ya 44 na kuwafanya waende mapumziko wakiwa mbele kwa mabao 2-1.

Bao la tatu la Uganda lilifungwa na Ivan Bogere huku Kenneth Semakula akifunga la nne dakika ya 72 baada ya kupiga 'frikiki' iliyokwenda moja kwa moja nyavuni baada ya kipa wa Tanzania kushindwa kuupangua.

Kipindi cha pili Ngorongoro Heroes ilifanya mabadiliko, lakini karata za Kocha Mkuu wa timu hiyo, Jamhuri Kihwelo 'Julio', jana hazikuchangika vizuri na kuwafanya Waganda hao kubeba ubingwa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >